MID WEEK JACKPOT!
TZS. 567,947,180
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**BoT yatoa ufafanuzi kuadimika kwa dola**
UKURASA 3


Nipashe Spotika
WACHEZAJI WA5 WANAOLIPWA ZAIDI LALIGA 2022-23

UKURASA 11

Nipashe
Jumatatu Mei 1, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581297
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

# Mkulima kuwashtaki wabadhirifu waliotajwa ripoti ya CAG

• **Wamo** mawaziri na wakuu mashirika; wanasheria wamuunga mkono...*Ukurasa 2*


Mkulima Thomas Nkola

## Sakata la mwalimu kufungiwa ujira kisa kufuatilia stahiki za uhamisho

UKURASA 7

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**NECTA YATOA NAMBA MAALUM KUNASA WANAOFANYA UDANGANYIFU**

BARAZA la Mitihani (NECTA) limesema kuwa kesho Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita...

UKURASA WA 15

**JELA MIAKA 30 KWA KOSA LA KUBAKA**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi mkoa Geita imemhukumu Elisha James (47), mkazi wa Kijiji cha Kishimbazobe...



MEI MOSI

## Matarajio waliyonayo wafanyakazi kutoka kwa Rais Samia leo

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA KUSUKWA UPYA MICHUANO CAF UK.24

**KATUNI** UK.6



Mwakilishi wa shirika la Kazi Duniani nchini (ILO), Getrude Sima akionyesha tuzo waliyotunukiwa na OSHA kwenye maadhimisho ya siku ya Usalama na Afya Mahala pa kazi duniani yaliyofanyika mkoani Morogoro mwishoni mwa wiki. ILO ilitunukiwa tuzo hiyo kwa kuwa taasisi iliyo mstari wa mbele katika kubadilishana taarifa za masuala ya usalama na afya nchini, kikanda na kimataifa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mkulima atinga kortini kuwashtaki aliotaja CAG kuhusika ubadhirifu

**Na Waandishi Wetu**

THOMAS Nkola, mkazi wa Mtaa wa Majengo wilayani Maswa mkoani Simiyu, ameamua kufungua kesi mahakamani kushinikiza kuwajibishwa kwa watendaji wa serikali waliotajwa kuhusika na ubadhirifu wa mabilioni ya shilingi katika ripoti ya mwaka 2021/22 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Katika mazungumzo na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Nkola (57), alisema ameamua kufungua kesi hiyo kwa kuzingatia Ibara ya 27(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Kifungu cha (1) cha ibara hiyo kinatamka: "Kila mtu ana wajibu wa kulinda mali asilia ya Jamhuri ya Muungano, mali ya Mamlaka ya Nchi na mali yote inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine."

Pia inatamkwa katika kifungu cha (2) cha ibara hiyo kuwa: "Watu wote watatakiwa na sheria kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhilifu, na kuendesha uchumi wa taifa kwa makini kama watu ambao ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya taifa lao."

Nkola alisema kuwa tangu Aprili 6 mwaka huu ilipowasilishwa bungeni Ripoti ya CAG kwa mwaka 2021/22, kumekuwa na zogo kubwa. Vyama vya siasa vinalalamika na vingine kutaka kufanya maandamano. Asasi za kiraia na wananchi wa kawaida pia wanalalamika.

"Wananchi tulitarajia hatua za haraka zingechukuliwa, hasa kupitia Bunge letu, lakini huenda kuna ushawishi wao kupitia nafasi walizonazo na hata fedha nyingi walizotuibia. Hawachukuliwi hatua. Vyombo husika vya kuchukua hatua, tunaona vinatupiana mpira.

"Mheshimiwa Rais anahangaika huku na kule kutafuta fedha lakini watanzania wenzetu wachache wanachota fedha na kufanya ubadhirifu. Wanaliacha taifa letu katika ufukara.

"Kwa kuwa fedha za wananchi zimetafunwa, nimeamua kama mwananchi, kwa kutumia haki yangu ya kikatiba, Ibara ya 27(1) na (2), kufungua kesi mahakamani," Nkola alisema.

Mkulima huyo alidai Ijumaa iliyopita, alifika katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini kutaka kufungua kesi mahakamani, lakini kuna kipengele kilileta dosari, akashindwa. Kesi yake ni ya kikatikba. Inasikilizwa na Mahakama Kuu.

"Mwanasheria wangu anakirekebisha. Kufikia Jumanne kesi itakuwa imeshafunguliwa mahakamani. Nimeamua kuwashtaki mawaziri, wakuu wa taasisi na mashirika ya umma na wakuu wa kampuni binafsi waliotajwa katika Ripoti ya CAG," alisema.

Nkola amechagua mawaziri kadhaa, wakuu wa mashirika mawili ya umma, watendaji wa Benki Kuu ya Tanzania na wakuu wa kampuni binafsi (kwa sasa hatutaja majina). Anadai wametajwa kusababisha hasara ya jumla ya Sh. trilioni 8.4 katika ripoti hiyo ya CAG.

"Katika uchambuzi wangu, sikuweza kubainisha watu wote waliotajwa na CAG kusababisha hasara kwa serikali. Hao niliowataja wamesababisha hasara ya Sh. trilioni 8.4.

"Watanzania wengine waungane nami kuwashtaki wengine ambao wamelisababishia hasara taifa na ikiwezekana kulishtaki Bunge kwa kushindwa kuwawajibisha kwa mujibu wa Katiba.

"Kuendesha kesi hizi ni gharama kubwa. Hadi sasa nimepata wakili mmoja tu. Ninaomba watanzania wanichangie ili tulete nidhamu katika matumizi ya fedha za umma.

"CAG anaripoti kila mwaka fedha zimeliwa, huko serikalini ni kama wanalindana. Hawachukuliwi hatua. Sasa ni wakati wa kutetea taifa letu na kutoa fundisho kwa watu wanaokula fedha zetu.

"Tumsaidie Rais wetu. Juzi baada ya kubadidhiwa ripoti ya CAG, alitamka neno baya mno dhidi ya hao wanaotuibia. Tuna kila sababu kumsaidia Rais wetu," alisema Nkola na kuomba ulinzi ili afanikishe azma hiyo bila kikwazo kiuslama.

**WANASHERIA WALONGA**

Nipashe ilipomtafuta Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, kuzungumzia suala hilo, alimpongeza Nkola kwa hatua hiyo.

Aliiita ni hatua nzuri kwa kuwa watu wamekuwa wakitajwa kila mwaka na CAG kufuja mali ya umma pasi na hatua zozote za kisheria kuchukuliwa.

Anna ambaye kitaaluma ni mwanasheria, alisema pamoja na uamuzi huo Nkola, anahitaji kupata mwanasheria mzuri ili amsaidie kuijenga kesi hiyo.

"Amechukua uamuzi mzuri kwa sababu utaifanya jamii ione kuwa kuna watu wana uchungu na rasilimali za nchi na wasingependa kuona zinatumika vibaya. Anahitaji mwanasheria mzuri ili amsaidie kuitengeneza kesi hiyo," alisema.

Wakili wa Kujitegemea, Amani Mkwama akizungumza na Nipashe jijini Arusha jana kuhusu suala hilo, aliutaja uamuzi wa Nkola ni wa kizalendo.

"Amechukua uamuzi sahihi, lakini njia aliyotumia siyo sahihi. Anataka mahakama iwafilisi, hili halitafanyika. Kwa kuwa hii ni kesi ya kikatiba, anapaswa aiombe Mahakama Kuu itamke kwamba matendo hayo ya watendaji wa serikali yanakinzana na Katiba ya nchi Ibara 27(1) na (2).

"Ni mawazo mazuri. lengo lake ni kuamsha hisia. Jamii ione ukubwa wa tatizo lililopo. Ni suala ambalo linaiamsha serikali, ione umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya watendaji wake waliotajwa kufanya ubadhirifu. Imejengeka kasumba ya watendaji kula fedha za umma bila hatua kuchukuliwa dhidi yao," alifafanua.

MTIHANI KIDATO 6, UALIMU

# NECTA yatoa namba maalum za kunasa wanaofanya udanganyifu

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani (NECTA) limesema kuwa kesho Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita utaanza huku likitoa namba maalum ya kupokea taarifa za udanganyifu wa aina yoyote utakaofanyika katika vituo vya mitihani ambayo wadau wanapaswa kuitumia.

Katibu Mtendaji wa Baraza, Dk. Said Ally Mohamed, alitangaza hilo jana mkoani Dar es Salaam na kuitaja namba hiyo kuwa ni 0759 360 000.

"Baraza linaomba wadau wote kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu. Kuhusu taarifa za kuwapo wa via viashiria vya udanganyifu katika vituo vya mitihani tafadhali mawasiliano yafanyike Baraza la Mtihani kwa namba hiyo, " alisema.

Kiongozi huyo alisema mtihani huo utaanza kesho hadi Mei 22 mwaka huu. Watahiniwa 106,955 wamesajiliwa kuufanya ambapo kati yao, wa shule ni 96,914 na wa kujitegemea ni 10,041.

Alisema kati ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa, wanaume ni 53,324 sawa na asilimia 55 na wanawake ni 43,590 sawa na asilimia 45.

"Watahiniwa wenye mahitaji maalum ni 181. Kati yao, 114 ni wenye uoni hafifu, 14 ni wasioona, 28 wenye ulemavu wa viungo vya mwili na mmoja ni mwenye mtindio wa akili," alifafanua.

Alisema kuwa kati ya watahiniwa wa kujitegemea 10,041 waliosajiliwa, wanaume ni 6,248 sawa na asilimia 62 na wanawake ni 3,793 sawa na asilimia 38. Mmoja ana uoni hafifu.

Pia alisema kutafanyika mitihani ya ualimu ambayo itakayomalizika Mei 16 mwaka huu, ikihusisha watahiniwa 8,906. Kati yao, 2,344 ni wa ngazi ya stashahada na 6,562 ni wa ngazi ya cheti.

"Ngazi ya stashahada wanaume ni 1,438 sawa na asilimia 61 na wanawake ni 906 sawa na asilimia 39. Watahiniwa ngazi ya cheti, wanaume ni 2,885 sawa na asilimia 44 na wanawake ni 3,677 sawa na asilimia 56. Wenye uoni hafifu wapo watatu kwa ngazi ya stashahada na wanne ngazi ya cheti. Tuna mtahiniwa mmoja asiyeoona," alisema.

Dk. Mohamed alisema kuanzia kesho hadi Mei 15 mwaka huu, kutafanyika mtihani wa marudio wa kidato cha nne ukihusisha wanafunzi 337 ambao matokeo yao yalifutwa mwaka 2022 kutokana na udanganyifu.

"Uamuzi wa watahiniwa kurudia mitihani umezingatia kuwa zaidi ya asilimia 60 ya watahiniwa waliofanya udanganyifu huo, chanzo kilitokana na mipango iliyofanywa na kuratibiwa na vituo husika kwa kushirikiana na wamiliki wa shule, wakuu wa shule, walimu na wasimamizi wa mitihani.

"Baraza limekwishawasilisha taarifa ya wale wote waliohusika naa udanganyifu huo kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe," alisema. Aliongeza kuwa vituo vya awali vilivyotangazwa kufungiwa kuwa vituo vya mitihani ya taifa vilikuwa vitatu, lakini baraza limejiridhisha kuwapo ukiukwaji mkubwa wa taratibu za uendeshaji mitihani ya kidato cha nne kwa vituo vingine viwili.

Alivitaja vituo hivyo kuwa ni Shule ya Sekondari Thaqaafa iliyoko mkoani Mwanza na Shule ya Sekondari Twibhoki ya mkoani Mara ambazo zimefungiwa kuwa vituo mpaka hapo watakapojiridhisha kuwa salama.

# BoT yatoa ufafanuzi kuadimika kwa dola

**Na Jenifer Gilla**

WAFANYABIASHARA wanaoagiza bidhaa nje ya nchi, ikiwamo China, wamelalamikia kuadimika kwa dola za kimarekani kuwa kunakwaza upatikanaji wa bidhaa kwa wakati, hivyo kuathiri biashara zao.

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imekiri kuwapo dosari hiyo, ikiitaja imetokana na changamoto ya jumla ya ukwasi wa fedha za kigeni katika mzunguko ulimwenguni iliyosababishwa na athari za ugonjwa wa UVIKO-19 na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Nipashe ilitembelea baadhi ya benki jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kutaka kufahamu ukweli wa malalamiko hayo, ikibaini kuwa nyingi kwa sasa haziruhusu mfanyabiashara abadili zaidi ya dola 1,000. Wanafanya hivyo ili wateja wengi wapate huduma kwa kuwa dola zimekuwa adimu.

Mmoja wa wafanyabiashara wanaouza vifaa kwa ajili ya michezo ya watoto, Doroth James alisema tangu Januari mwaka huu upatikanaji wa dola umekuwa mgumu. Umekuwa kikwazo kwa wafanyabiashara.

Alisema kuna kipindi inamchukua siku mbili kupata dola 5,000 anapohitaji kwa ajili ya kulipia mzigo China kwa kuwa benki anazokwenda wanamwambia wanabadili dola 1,000 tu kwa kila mteja kwa siku.

Mfanyabiashara wa nguo za watoto Kariakoo jijini, Rhoda Enea, alisema wakati wa sikukuu za Pasaka na Eid el Fitr mwezi huu, mzigo wake uliuzwa kwa mtu mwingine baada ya kushindwa kuulipia kwa wakati kutokana na kukosa dola.

Mfanyabiashara wa viatu vya kiume maeneo ya Sinza wilayani Kinondoni, Leonard Jacob, alisema: "Wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao hupata wateja kutoka nchi jirani kama Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambao hununua bidhaa na kulipa kwa dola.

"Sasa hawa ndio wanawauzia wenzao wanaotaka dola kwa bei ya juu tofauti na benki, jambo linaloikosesha serikali mapato."

**MAJIBU YA BOT**

Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa BoT), Alexander Ng'winamila, katika majibu yake kwa Nipashe, alisema kumekuwa na changamoto ya jumla ya ukwasi wa fedha za kigeni kwenye mzunguko ulimwenguni. Imesababishwa na UVIKO-19 na vita kati ya Russia na Ukraine.

Kwa kutambua hilo, Ng'winamila alisema: "Benki Kuu inaendelea kuhakikisha sekta ya fedha inaendelea kuwa imara ili kuhakikisha hakuna mkwamo wa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ukwasi wa fedha za kigeni."

Alisema biashara ya fedha za kigeni nchini inaongozwa na nguvu ya soko, yaani kiasi cha ukwasi wa fedha za kigeni kilichopo katika mzunguko kulinganisha na uhitaji wa fedha za kigeni.

Alisema BoT haizipangii benki za biashara nchini kiwango cha kuwauzia wateja wake kwenye soko la rejereja. Alizitaja takwimu zilizopo zinaonyesha kutokuwapo mkwamo kutoka kwa wafanyabiashara waagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni.




Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Alliance One Tobacco Tanzania Ltd, Blasius Lupenza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Ephraim Mapoore akimkabidhi T-shirts zenye thamani ya shilingi milioni 10 Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Fatuma Mwasa zitakazotumika wakati wa Sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani zitakazofanyika kitaifa mkoani humo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Matarajio ya wafanyakazi kutoka kwa Rais Samia leo

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani leo, wadau wa sekta ya ajira nchini wameiomba serikali kuboresha mifumo ya utendaji kazi ili jamii iishi katika mazingira mazuri ikiwamo ya kiuchumi.

Sherehe za Siku ya Wafanyakazi kitaifa zinafanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro ikibebwa na kaulimbiu 'Mishahara Bora na Ajira za Staha ni Nguzo ya Maendeleo kwa Wafanyakazi' huku mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mwalimu wa Sekondari Mbeya, Festo Kasanga alisema serikali inapaswa kuongeza motisha kwa wafanyakazi, kwa kuwawekea mazingira mazuri, kuwasikiliza na kutekeleza makubaliano kwa mujibu wa sheria na mkataba wa kazi.

Alifafanua kuwa walimu wanaofundisha shule za msingi na sekondari wengi wao wanaishi katika mazingira duni na kuhitaji motisha ya mishahara na kuwaboreshea mazingira ya ufanyaji kazi wao.

Daktari wa Zahanati ya Kijiji cha Mgowelo, Musa Omari, aliomba serikali kuwakumbuka madaktari wa vijijini akidai wengi wao wanafanya kazi katika mazingira magumu ikiwamo kuishi kwenye nyumba zenye ubora hafifu.

Katibu Mkuu Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUKTA), Hery Mkunda, alisema malalamiko makubwa ya wafanyakazi wengi nchini ni kutaka kupewa mishahara bora na ajira zenye staha.

Alisema wafanyakazi wengi wanafanya kazi bila mikataba, hali inayowafanya washindwe kupata haki zao na wengine hata kudhulumiwa inapotokea shida na mwajiri wake.

Alibainisha kuwa wamekuwa wakipokea malalamiko mengi kutoka kwa wafanyakazi kutoka kwenye taasisi mbalimbali na sekta binafsi wakitumikishwa kwa muda mrefu bila kupewa mkataba akidai kuwa jambo hilo lipo kinyume cha sheria.

Pia aliwataka waajiri nchini kujali maslahi ya wafanyakazi na kufuata makubaliano kwa mujibu wa mikataba waliyokubaliana, kutowanyanyasa wafanyakazi na kuwalipa fedha za kufanya kazi nje ya muda.

**NENO LA ILO**

Wakati huo huo, Shirika la Kazi Duniani (ILO) limetaja njia bora za kufanyika ili kutoa kazi bora, kukabiliana na ukosefu wa usawa kazini na kupunguza umaskini kwa jamii ili ijikimu na kujenga maisha yao ya baadaye.

Ujumbe uliotolewa na Mkurugenzi wa Shirika hilo, Gilbert Houngbo, unataja njia hizo kuwa ni kufanyika mabadiliko ya kimuundo ya muda mrefu ikiwamo kubuni teknolojia mpya itakayosaidia kuongeza ajira na kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema pia ni muhimu kuwekwe nguvu kwenye taasisi na mashirika ya wafanyakazi ili mazungumzo ya kijamii yawe ya ufanisi na yenye nguvu na tukagua sheria na kanuni zinazoathiri ulimwengu wa kazi, ili ziwe muhimu na za kisasa, kulinda wafanyakazi na kusaidia biashara endelevu.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliwaomba wananchi kujitokeza kwa wingi katika Uwanja wa Jamhuri ili kumsililiza Rais atakayekuwa mgeni rasmi.

*** Imeandikwa na Jenifer Gilla, Halfan Chusi (DAR) na Ashton Balaigwa (Morogoro).**

# Mkomazi yajipanga ongezeko la watalii

**Na Mwandishi Wetu,** SAME

HIFADHI ya Taifa Mkomazi wilayani Same mkoani Kilimanjaro, imetekeleza kwa asilimia 100 miradi ya uboreshaji miundombinu na kuifanya kuwa miongoni mwa hifadhi zenye mazingira rafiki kwa watalii.

Akizungumza katika mahojiano maalumu hifadhini hapo, Mkuu wa Hifadhi hiyo, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi (ACC), Emmanuel Moirana, alisema miradi iliyotekelezwa na kukamilika ni pamoja na ujenzi/ukarabati wa barabara, ujenzi wa kiwanja kidogo cha ndege, mageti ya kuingia hifadhini na ya kukusanyia mapato.

"Mkomazi ni moja ya maeneo nufaika na miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 (TCRP).

"Lengo ni kuboresha miundombinu na kukuza utalii na mapato yatokanayo na utalii hifadhini, pamoja na kuweka mazingira rafiki kwa watumishi kufanya kazi mfano, ofisi, makazi na vitendea kazi," alisema.

Miradi iliyokamilika ni lango la kukusanyia mapato, nyumba tano za watumishi, maeneo mawili ya maegesho ya magari na vyoo viwili vya kisasa, maeneo ya kupumzikia wageni (shades), ukarabati wa viwanja viwili vya ndege, ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilometa 146 na vivuko.

Lengo kuu la miradi hiyo ni kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya kupokea ongezeko la watalii kutokana na janga la ugonjwa Corona na uzinduzi wa filamu ya Tanzania 'The Royal Tour' iliyoandaliwa na kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Kamishna Msaidizi Moirana alisema, sasa wageni wanaweza kufika hifadhini kwa kutumia ndege, kwa kuwa awali hapakuwapo kiwanja cha ndege rasmi kwa shughuli za utalii.

Hifadhi ya Mkomazi imesheheni vivutio mbalimbali kama ndege wa aina mbalimbali, wanyama pori wakiwamo faru weusi ambao wako hatarini kutoweka duniani.

Tafsiri kamili ya Mkomazi ni kijiko cha kipare kisichokuwa na tone lolote la maji. Huenda neno hilo pia linathibitisha hali halisi ya upatikanaji wa maji katika eneo hilo ulivyo mgumu, pia hifadhi hiyo imewahi kutembelewa na Mjukuu wa Malkia Elizabeth II wa Uingereza, Prince William.

Hifadhi ya Mkomazi ni miongoni mwa hifadhi 22 za Taifa zilizo chini ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi ambayo inapatikana katika mikoa miwili ya Kilimanjaro na Tanga ikiwa ndani ya Wilaya za Same na Lushoto, ilianzishwa kama Pori la Akiba lililomegwa kutoka katika Pori kubwa la Akiba la Ruvu mwaka 1951.

Kwa mujibu wa TANAPA, hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilomita za mraba 3,245 na ilipendekezwa kuwa Hifadhi ya Taifa kwa misingi ya kunusuru maeneo na rasilimali zilizomo kutokana na matumizi yasiyoendana na uhifadhi endelevu.

# Wataka FCT kutoa amri kukazia katazo uuzaji wa Tanga Cement

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wanaopinga ununuzi wa Kampuni ya Saruji ya Twiga kununua hisa za Kampuni ya Saruji ya Tanga, wamewasilisha maombi ya kutaka Baraza la Ushindani wa Biashara (FCT) kukazia hukumu iliyotoa juu ya katazo la kuendelea kwa mchakato huo.

Kwa mujibu wa wadau hao, kitendo cha Tume ya Ushindani (FCC) kuendelea na mchakato huo ilhali kuna zuio la kufanyika kwa jambo hilo ni kinyume cha sheria zinazosimamia masuala ya miunganiko ya kampuni kwa kuwa suala hilo lilishasimamishwa.

Suala la kununuliwa kwa hisa na kufanya muunganiko wa kampuni kupitia Scancem International DA ambayo ni sehemu ya Heilderberg Cement inayomiliki Twiga Cement, lilipingwa FCT na wadau wa saruji ambao ni kampuni ya Saruji ya Chalinze, Chama cha Watumiaji wa Saruji na Peter Heller kwamba kunaweza kuleta athari katika soko la saruji. Walisema iwapo Twiga itaruhusiwa kununua hisa hizo, kuna uwezekano wa kuwapo na ukiritimba katika soko kwa kuwa Twiga Cement kupitia muungananiko huo, itakuwa na zaidi ya asilimia 68 katika soko. Hali hiyo, walisema inaweza kusababisha upangaji wa bei, hivyo watumiaji wa bidhaa kushindwa kumudu gharama.

Akizungumza mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Wakili Mkuu wa Kampuni ya Mawakili ya MSL Attorneys wanaowatetea wadau hao, Melkisedeck Lutema, alisema kitendo cha FCC kuendelea na mchakato wakati kuna uamuzi wa kisheria kuzuia suala hilo, ni ukiukwaji wa kisheria.

"Katika uamuzi uliotolewa Desemba 22, 2022 na FCT chini ya Mwenyekiti Jaji Salma Maghimbi, iliamuliwa kwamba mchakato huo usitishwe lakini cha ajabu Februari 28, 2023, FCC waliendelea kwa kutoa hati ya muunganiko. Kwanini FCC wasichukuliwe hatua za kisheria kwa kudharau na kukaidi amri halali ya chombo kilichowekwa kisheria?

"Kisheria, jambo lolote likitolewa uamuzi katika chombo chochote kilichowekwa kisheria, halipaswi kuendelea kufanyika. Na suala la muunganiko wa Twiga na Tanga Cement limezuiwa na hakuna mtu aliyepinga kwa kukata rufani, kuomba mapitio. "Ni muhimu ikaeleweka kuwa uamuzi uwe sawa au si sawa na hakuna mtu aliyeupinga ni lazima uheshimiwe. Kwa hiyo, mtu yeyote anayeendelea anakiuka sheria na anapaswa kuchukuliwa hatua. Kwa hili tumeomba FCT kukazia hukumu ili uvunjaji huu wa sheria usiendelee," alisema Lutema. Lutema alisema suala la uuzwaji wa hisa na muunganiko wa kampuni kama unavyoendelea, umegubikwa na usiri mkubwa, hali inayoibua maswali mengi kwanini Twiga Cement pekee inunue Tanga Cement badala ya kualika wadau na kampuni zingine kujitoleza na kuonyesha nia ya kununua hisa hizo. "Nini kimejificha nyuma ya pazia kutaka Twiga Cement pekee ipewe kipaumbele wakati duniani kuna kampuni nyingi za kuzalisha saruji? Kama kweli tunataka kuwe na ushindani wa haki, litolewe tangazo kualika wadau mbalimbali ili washindane na Twiga badala ya upekee unaofanywa kwa Twiga," alisisitiza.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Profesa, Joyce Ndalichako akimkabidhi tuzo Mkuu wa kitengo cha Ulinzi, Usalama na Mwendelezo wa Biashara wa Benki ya CRDB, Misana Mutani wakati Benki ya CRDB ikitunukiwa tuzo tatu ambazo ni mshindi wa kwanza katika kundi la benki na taasisi za fedha katika utekelezaji wa sera za Osha, tuzo nyingine ni ya ufanisi katika utoaji huduma bora unaozingatia afya na usalama wa kazi kwa benki na ile ya kamati bora ya Osha katika huduma za kibenki, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Morogoro.**PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

# CRDB yapongezwa kujali usalama mahali pa kazi

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi nchini (OSHA) umeipongeza Benki ya CRDB kwa kuwa mfano kwa taasisi za kifedha katika kuzingatia suala la usalama na afya kwa wafanyakazi wake maeneo mbalimbali nchini.

Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda alitoa pongezi hizo jana wakati wa kilele cha Madhimisho ya Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Morogoro.

Mbali na pongezi hizo, benki hiyo pia ilipewa tuzo kwa kuzingatia suala hilo. "Ninaipongeza taasisi hii ya kifedha nchini kwa kuwa mfano katika kuzingatia suala zima la usalama mahali pa kazi. Ninapenda kuchukua nafasi hii kuzitaka taasisi zingine nazo ziige mfano huu ili kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi kwa wafanyakazi wao," alisema Khadija.

Alitaja lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha umma kuhusu usalama na afya ambayo wao wanaisimamia chini ya sheria namba tano ya mwaka 2003. OSHA imekuwa inafanya maadhimisho ili kuwakumbuka wafanyakzi waliopoteza maisha au kuathirika kutokana na maeneo yao ya kazi, pia kuonyesha namna bora ya kuboresha usalama sehemu za kazi na jinsi zinavyoweza kusimamiwa katika kuhakikisha usalama kwa wafanyakazi wote.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliyekuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo, alisema serikali inatambua na kuthamini masuala ya afya na usalama mahali pa kazi.

"Usalama na afya mahali pa kazi ni haki ya msingi ya kila mfanyakazi nchini na ndiyo sababu Rais amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha nguvu kazi ya taifa inalindwa," alisema Ndalichako. Waziri Ndalichako alisema serikali kupitia OSHA inaendelea kusimamia kwa karibu sheria namba tano ya afya na usalama mahali pa kazi ya mwaka 2003 kwa lengo la kuhakikisha maeneo yote ya kazi yanakuwa na mifumo madhubuti ya kuwalinda wafanyakazi dhidi ya ajali au magonjwa.

Alizipongeza taassisi zote na wadau wengine kwa ujumla walioshiriki katika maadhimisho hayo ikiwamo Benki ya CRDB, akiwataka wote waliopata fursa ya kushiriki kuongeza ufanisi zaidi katika kusimamia suala la usalama na afya mahali pa kazi kwenye taasisi zao.

Mkuu wa Kitengo cha Ulinzi, Usalama na Mwendelezo wa Biashara wa Benki ya CRDB, Misana Mutani alisema ufanizi mzuri wa benki hiyo ndiyo uliozaa matunda ya wao kupewa tuzo tatu katika kuzingatia afya na usalama mahali pa kazi kwa wafanyakazi. Mutani alisema benki siyo tu kuwa inazingatia usalama wa wafanyakazi wake pekee, bali pia hata kwa jamii inayoizunguka kwa maana ya wateja na wageni wanaotembelea maeneo ya benki hiyo, Inahakikisha wapo salama.

Mbali na kuzingatia afya na usalama mahali pa kazi, Mutani alisem benki hiyo pia imeendesha mbio za marathon, maarufu CRDB Marathon ambazo kila mwaka zimekuwa zinafanyika kwa mafanikio makubwa, zikilenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuisaidia jamii, hususani watoto wenye matatizo ya moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwetu (JKCI).

# Waziri asema idadi kubwa wenye usonji hawatibiwi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema katika vizazi hai milioni 2.4 kila mwaka, watoto 15,000 huzaliwa na tatizo la usonji.

Kati ya watoto hao 15,000, asilimia 10 sawa na watoto 1,500 ndio wenye tatizo kubwa.

"Kwa bahati mbaya takwimu za watoto wanaopata huduma kwa miaka 10 ni watoto 2,000 kati ya 15,000 wanaozaliwa na tatizo hili kila mwaka, hivyo ninaomba nitoe rai kwa wazazi kuwapeleka hospitalini kupata huduma za matibabu," amesema.

Waziri Ummy aliyasema hayo jana wakati wa kuhitimisha mbio zilizoandaliwa na Taasisi ya Lukiza kwa lengo la kuchangisha fedha za kutoa elimu kwa jamii na kusaidia watoto wenye tatizo hilo nchini.

Alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa kwa kila vizazi 160 duniani, mtoto mmoja anazaliwa na usonji.

Ummy aliwataka wananchi kupunguza unyanyapaa kwa watoto wenye usonji ili kusaidia kuboresha maisha yao.

Pia aliitaka jamii kutowabagua bali kushirikiana nao na kuhakikisha wanapata huduma zote muhimu.

Ummy alisema nchini zipo shule 18 zilizosajiliwa kutoa huduma za mahitaji maalum ikiwamo usonji na walimu 157 ingawa hawatoshi.

Ummy aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto hao katika shule maalum ili wapate huduma na kufundishwa mambo mbalimbali.

Alisema serikali inayatambua matatizo ya upatikanaji wa huduma za watoto wenye usonji na inaendelea kuboresha na kupanua huduma zao.

Alisema serikali imeanzisha mafunzo ya ngazi ya stashahada ili kupata wataalamu wa kutoa elimu na huduma kwa watoto wenye mahitaji maalum.

Aliwatia moyo wazazi na walezi wanaolea watoto hao wenye usonji kwa sababu serikali inaendelea kuyafanyia kazi matatizo yote yanayowakabili.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Lukiza, Hilda Nkabe, aliiomba serikali kuongeza wataalamu wa kuwahudumia watu wenye usonji ili kupunguza unyanyapaa ndani ya jamii au kugharimu kufuata matibabu nje ya nchi.

Alisema watoto wanaopatia huduma za matibabu na masomo, wanaweza kufanya shughuli zao muhimu za kawaida tofauti na wale ambao hawapewi huduma yoyote.

# Viongozi wa dini, mila wataka marekebisho Sheria ya Ndoa

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

VIONGOZI wa dini na mila wameiomba serikali kurekebisha Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, wakiitaja ina shida katika umri wa kuolewa.

Wamesema sheria hiyo ilitungwa kulingana na wakati huo. Sasa ni wakati mwafaka kuona namna nzuri ya kutekeleza mahitaji ya watu ya umri wa kuolewa uwe kuanzia miaka 18.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa wakati wa Kongamano la Kitaifa la Sheria ya Ndoa lililowashirikisha wabunge, wanazuoni, viongozi wa serikali, dini, mila na asasi za kiraia zinazojihusisha na masuala ya sheria na utetezi wa haki za binadamu.

Sheria hiyo inatoa mwanya kwa mtoto mwenye umri wa kuanzia miaka 14 kuingia katika ndoa.

Mwakilishi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Yonas Mlewa, alisema ni lazima serikali ifanye marekebisho ya sheria hiyo kwa kuwa inakwenda kinyume cha maagizo ya Mungu.

"Umri lazima uanzie miaka 18, ndoa ni ya watu wazima, mwanamke na mwanamume wanaoingia kwenye ndoa wanapaswa kuwa na ukomavu wa kiakili, mtoto hana uwezo wa kuhimili, kuyapokea na kuyatatua matatizo," alisema Padri Mlewa.

Alisema viongozi wa dini wanakutana na kesi nyingi za ndoa na wakapofanya vikao vya upatanisho, wengi wanasema walikuwa hawajui nini maana ya ndoa.

Kadhi ya Mkoa wa Dodoma, Kisusu Mvumbo alisema jambo hilo lisipotazamwa vizuri, litaleta athari kubwa katika jamii.

Alisema sheria hiyo ni mojawapo ya kisababishi cha ongezeko la watoto wa mitaani; kwamba wengi wanaingia katika ndoa pasipo kufahamu undani wake. Muda mfupi ndoa huvunjika na watoto kuingia mitaani.

"Umri lazima uongezwe uwe kuanzia miaka 18. Mbali na suala la miaka pia tunapaswa kuangalia haki za kinamama kutelekezwa, wengi wanapewa mimba, baada ya muda mfupi wanatelekezwa, unakuta mitaani watoto wamezagaa," alisema Mvumbo.

Askofu wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Jimbo la Kati Dodoma, Richard Khaniki, alisema serikali inapaswa kuweka mfumo mzuri wa kuwalinda watoto. Alisema watoto ndiyo wanaotegemewa kuongoza taifa, hivyo wasipowekewa misingi mizuri ya kulindwa ni sawa na kuliangamiza taifa la baadaye.

Theresia Mhanjala, kutoka Taasisi ya Macho kwa Jamii inayojihusisha na utetezi wa haki za jamii alisema: "Marekebisho yafanyike, umri uwe kuanzia miaka 18, lengo ni kumuweka salama mtoto wa kike".

Makamu Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Dodoma, Chifu Mtupa, alisema: "Ninapendekeza umri wa kuolewa uwe miaka 18. Huko vijijini tunaona mengi, mtoto akilia na yeye (mama) analia, mtoto akijisaidia na yeye (mama) anaona kinyaa na anashindwa kumsafisha."

Chifu Zule Gama kutoka Ruvuma alisema: "Mimi nimekemea sasa vitendo vya ndoa za utotoni. Wanaoendelea kwa sasa ni suala la umaskini, sheria ibadilike kwa sababu itatujengea heshima".

Akihitimisha kongamano hiyo, Waziri wa Sheria na Katiba, Dk. Damas Ndumbaro, alisema zaidi ya watu 200 walitoa maoni. Serikali imeyapokea na inakwenda kuyachakata. Yatafika bungeni ili wabunge wafanye marekebisho kwa namna itakavyofaa.

# MSD yakutana na wadau kuboresha huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu**

BOHARI ya Dawa (MSD) Kanda ya Kati Dodoma, imekutana na wadau na wateja wake wakiwamo waganga wakuu, wafamasia na watendaji wa halmashauri kujadili uboreshaji wa huduma za afya na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa uhakika kupunguza kero kwa wananchi.

Katika mkutano huo wadau wamekubaliana kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan za maboresho sekta ya afya kwa vitendo kwa kutumia taaluma zao kutoa huduma stahiki.

Akizungumza jana wilayani Kondoa mkoani Dodoma, Meneja wa MSD Kanda ya Kati, John Sipendi alisema, lengo la bohari kurejesha mikutano hiyo ya pamoja na wadau ni kukubali kukosolewa, kujenga mazingira ya kupunguza changamoto za pande zote mbili, kubadilisha uzoefu na kukubaliana kufanya kazi kwa pamoja bila kutafuta mshindi kwa kuwa wote wanamhudumia mwananchi wa Tanzania.

Alisema, kikao kazi hicho kati ya watendaji wa MSD wa Kanda na Makao Makuu, wadau na wateja wake wakiwamo waganga wakuu wafamasia na watendaji wa halamshauri ni kuhakikisha wanajadili uboreshaji wa huduma za afya na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa uhakika kupunguza kero kwa jamii.

"Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano kati yetu na wadau wa afya mkutano huu umeazimia kuunga mkono jitihada za Rais Samia za amboresho sekta ya afya kwa vitendo kwa kutumia taaluma zetu kutoa huduma stahiki na kwa wakati," alisema.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Ally Gugu, alisema katika kikao hicho kikichoshirikisha watendaji wenye ngazi ya uamuzi wa Mkoa wa Dodoma na maeneo ya jirani, ikiwemo Singida na Manyara kwa pamoja wamejadili maboresho ya ufikishaji wa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma na namna ya kushirikiana kumpatia Mtanzania huduma bora za afya.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA
Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA
UTOAJI WA RISITI ZA EFD KWA WASAFIRISHAJI WA VIFURUSHI NA VIPETO

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuagiza wasafirishaji wote nchini wanaosafirisha vifurushi na vipeto kuwa, kwa mujibu wa **Sheria ya Usimamizi wa Kodi CAP.438 R.E 2019 Kifungu cha 36 (1)**, wanatakiwa kutoa risiti ya EFD kwa wateja wao.

Kwa tangazo hili mnafahamishwa kuwa, Mameneja wa TRA Mikoa yote na Wilaya zote wataanza zoezi la kufuatilia jambo hili kwa karibu na kuchukua hatua stahiki kuanzia **tarehe 1 Mei, 2023**.

Tangazo hili ni kwa ajili ya kuwakumbusha wahusika kutekeleza wajibu wao kwani Sheria ipo na inapaswa kutekelezwa pasipo shuruti.

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa namba za bure zifuatazo;- **0800-11 00 16** / **0800-75 00 75** / **0800-78 00 78** au kwa barua pepe: **huduma@tra.go.tz**. Pia tufuatilie katika mitandao ya Kijamii ya ***Facebook:TRA Tanzania, Twitter:@tratanzania***
***Instagram: tratanzania YouTube: TRA online TV.***

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

Imetolewa;

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hatuna cha kuwadai Simba, mmemaliza kwa heshima CAF

**WAWAKILISHI** wa nchi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Simba, Ijumaa usiku wakiwa ugenini, walimaliza safari yao ya kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kutolewa na Mabingwa Watetezi wa michuano hiyo, Wydad Casablanca ya Morocco kwa mikwaju ya penalti 4-3.

Miamba hiyo ilifikia hatua hiyo ya changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya kupata matokeo yanayofanana ndani ya dakika 90 kwa kila timu kushinda nyumbani bao 1-0.

Simba ndiyo iliyokuwa ya kwanza kupata matokeo hayo nyumbani katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Aprili 22, mwaka huu, kabla ya Ijumaa iliyopita Wydad nayo ikiwa kwenye Dimba lao la Mohammed wa Tano, Morocco kupata ushindi kama huo na ndipo changamoto ya mikwaju ya penalti ikipochukua nafasi yake na wenyeji hao kushinda 4-3.

Ingawa kutolewa ni kutolewa tu haijalishi ni kwa muda wa dakika 90 ama 120 au mikwaju ya penalti, lakini Simba inastahili pongezi kwa namna ilivyocheza soka la kuvutia na kuwaweka roho juu wapinzani wao huku ikiwanyamazisha mashabiki wa Wydad ambao wanasifika kwa kushangilia mwanzo mwisho.

Kwa hakika ilikuwa ni mechi ya robo fainali ya viwango dhidi ya mabingwa watetezi, Wydad ambao uwekezaji wake ni mkubwa zaidi ya mara 20 ya Simba huku ikiwa na wachezaji walitoka kucheza nusu Fainali ya Klabu Bingwa Dunia ukilinganisha na wawakilishi hao wa Tanzania ambao uwekezaji wake ni mdogo sana.

Lakini pia ikumbukwe si kila timu inaweza kutembelea pale Casablanca katika Uwanja wa Mohammed wa 5, ikafanikiwa kuunyamazisha umati ule wa mashabi 'vichaa wa soka' na kuwafanya washike tama muda mwingi wa mchezo huku wakiomba dua.

Tunakiri Simba ilistahili zaidi ya ilichopata kwani ilionyesha ukubwa mbele ya wakubwa kwenye michuano mikubwa na yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika, hivyo mashabiki, wachezaji, benchi la ufundi, viongozi wa klabu hiyo na Watanzania kwa ujumla, hawana budi kutembea kifua mbele na kurudi kujipanga zaidi kwa msimu ujao.

Tunasema hivyo hasa tukikumbuka namna Simba ilivyouanza msimu na jinsi timu inavyocheza kwa mabadiliko makubwa ikiwa chini ya Kocha Mbrazili Robertinho Oliveira ambaye alichukua katikati ya michuano hiyo.


Hii inatufanya tuamini kama Simba itaendelea kumpa nafasi kocha huyo na kusajili wachezaji wa daraja la juu atakaoenda nao kujiandaa kwa msimu mpya 'preseason', inaweza kutisha Afrika kwenye michuano hiyo na ile ya Super League itakayoanza baadaye mwaka huu.

Aidha, kwa hatua hii iliyofikia Simba kutoka kupigwa mabao 4-1 na TP Mazembe, 5-0 na Al Ahly misimu iliyopita ikiwa ugenini, kwa matokeo haya ya sasa hadi kutolewa kwa penalti inaonyesha inazidi kukua sambamba na soka la Tanzania kwa ujumla.

Ni wakati sasa kwa Simba kurudi kutazama wapi pakuboresha hususan wakimulika safu ya ulinzi na kiungo mkabaji ili kuifanya timu yao kuwa imara zaidi na kuendelea kubaki huko huko Ligi ya Mabingwa na kuiheshimisha nchi.

Kwa kiwango hicho cha Simba, Watanzania wote tunapaswa kujivunia soka letu kukua kitu ambacho kinaonyesha ishara nzuri katika ligi yetu kwa siku zijazo kama itaendelea kuboreshwa kila msimu na wadau kujitokeza kwa wingi kuwekeza katika soka la vijana kupitia klabu mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Deni Simba michuano CAF sasa limebaki kwa viongozi

Na Adam Fungamwango

**KWA** asilimia zaidi ya 90, hakuna mwanachama au shabiki wa Simba anayewalaumu wachezaji au kocha kutokana na kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu.

Kwanza kabisa ni kwa sababu wametolewa na Mabingwa Watetezi wa michuano hiyo, Wydad Athletic Club ya Casablanca kutoka nchini Morocco, tena kwa mikwaju ya penalti.

Ilizoeleka timu si za kutoka Afrika Kaskazini, Magharibi au Kusini, achilia mbali Mashariki na Kati zilizokuwa zikienda kule zikafungwa mabao machache, au kuwafanya mashabiki wa timu wasiwe na raha hadi mwisho wa mchezo. Simba imefanya hivyo, kwani dakika zilivyozidi kwenda mbele ndipo mashabiki 'vichaa wa soka' wa Wydad Casablanca walipozidi kuwa na wasiwasi kwa timu yao kama inaweza kufuzu kwenda hatua ya nusu fainali.

Baada ya matokeo ya jumla ya bao 1-1, Simba ikatolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 na safari yao ikaishia hapo.

Kwa jinsi michuano hii ilivyoanza na kikosi cha Simba kilivyokuwa awali pamoja na matokeo yake ya mwanzo hatua za makundi, hakuna aliyetegemea kuona hili lililotokea kuwapo leo.

Simba haikupewa nafasi hata ya kufuzu kwenye hatua za makundi, ikisemekana ina kikosi kibovu. Na hata ilipopoteza mechi zake mbili za mwanzo ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Horoya ya Guinea na Raja Athletic Club ya Casablanca Morocco mabao 3-0, ilionekana kabisa safari ingeishia kwenye makundi.

Hata hivyo, baada ya kuanguka, iliinuka ikajipangusa na kuanza safari yake taratibu ambayo ilikuwa ya kushangaza na yenye mafanikio.

Ujio wa kocha Roberto Oliveira raia wa Brazil haukupokelewa kwa furaha na wanachama na mashabiki wengi wa Simba, na hata alipoanza kuibadilisha na kucheza mfumo anaoutaka yeye huku wachezaji wakionekana hawakuuzoea, ilionekana kuwakera na kutaka atimuliwe mara moja.

Leo hii ukimfuata mwanachama na shabiki wa Simba na kumwambia Robertinho atimuliwe mtagombana.

Amekuta usajili umeshafanyika, alichofanya ni kutumia raslimali zilizopo zilizoitwa duni na kuzifanya ziwe kali, tishio na za mfano.

Ndiyo maana baada ya mechi ile, wanachama na mashabiki wengi wa Simba ukizunguka sehemu mbalimbali wanakwambia hawawadai wachezaji wala kocha. Walichofanya kinatosha kwa sababu awali hata wao hawakutarajia kama timu yao inaweza kufika pale na kuwachachafya Mabingwa wa Afrika.

Ukitazama umati uliofurika jana kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere kwa ajili ya mapokezi, unaakisi kile ambacho wanakisema mitaani na kwenye mitandai ya kijamii.

Binafsi, nimefurahishwa na mbinu za Robertinho pamoja na mapokeo ya mfumo mpya ya uchezaji kwa wachezaji wake.

Hata mimi siwadai wachezaji na kocha wa Simba, lakini nakwenda mbali zaidi na kusema wanaodaiwa sasa ni viongozi.

Kikosi cha Simba ni finyu sana, kina wachezaji wasiopungua 13 au 14 tu ambao wana uwezo wa kucheza mechi za kimataifa na si vinginevyo.

Ndiyo maana utaona kocha Robertinho ni mgumu kufanya mabadiliko kwa sababu ameshaona viwango vya wachezaji wake waliobaki.

Ukiangalia mechi nyingi za Simba au ya Wydad Casablanca, Yanga, na zingine wapinzani wao wanaweza kubadilisha wachezaji kuanzia watano kwa muda muafanka, lakini wenyewe wamekuwa hawabadilishi labda mpaka mwishoni. Tena ni mmoja au wawili na wanaoingia siyo kama ni bora kuliko aliyetoka.

Nadhani kama Simba ingekuwa na wachezaji wengi bora kiasi kwamba anaweza kutoka hata Clatous Chama na Saido Ntibazonkiza, wakaingia wengine wenye uwezo kama wao, zaidi au pungufu kidogo au Mzamiru Yassin na Sadio Kanoute wangekuwa mbadala wao, hata Shomari Kapombe na Mohamed Hussein wangepatikana wanaofanana nao kidogo, saa hizi timu ingekuwa imetinga nusu fainali.

Nimemsikia Afisa Mtendaji Mkuu, Imani Kajula, akisema watasajili wachezaji bora msimu ujao. Cha kuwakumbusha tu wasifanye tena makosa ya kusajili wachezaji wa kuja kukaa benchi na kuwatazama wenzao kama mapambo au maua. Wasajili wachezaji wa kukifanya kikosi kiwe imara na kipana, akitoka mtu aingie mtu na nusu na si kama hivi sasa. Hiki ndicho wanachodaiwa viongozi wa Simba na wanachama na mashabiki wao hivi sasa.

# JICHO KWA MFANYAKAZI SIKU YAO...

# Simulizi ya mateso mwalimu aliyezuiwa mishahara, kisa kudai haki za uhamisho

## - DED: Sijui lolote; Ofisa Utumishi amtetea, DEO agoma
## - Maisha yamkaba, chama walimu yampigania kortini

**Na Neema Hussein,** ALIYEKUWA WILAYA TANGANYIKA

LEO ni kilele cha Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani. Matarajio na kioo kilichoko ni shamrashamra kimataifa na kitaifa, serikali imetenda mengi kuwaboreshea wafanyakazi, ikiwamo Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya mwaka 2004.

Kama ilivyo methali kizuri hakikosi kasoro, ndipo kunaangukia mkasa kutoka mkoani Katavi, matendo ya 'uhusiano kazini' yanayotoa swali kati ya mwalimu na mwajiri wake, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, akiwa na simulizi ya kina

anapohojiwa na Nipashe kwamba mshahara wake umezuiwa, sababu kuu kudai stahiki zake za uhamisho kwenda kituo kipya cha kazi.

Mwalimu Ndebile Malcom, aliyekuwa akifundisha Shule ya Msingi Mpembe iliyoko Halmashauri ya Wilaya Tanganyika, anasimulia mnamo Machi mwaka jana, alipata uhamisho kwenda shule ya msingi Mwikang'ombe, wilaya hiyohiyo Tanganyika.

"Baada ya kupata barua hiyo ya uhamisho kama taratibu zinavyoelekeza nilienda kuripoti, nikarudi, nikaandika barua ya kuomba stahiki zangu, kama kanuni na sheria zilivyo husika niliendelea kwenda katika kituo changu kipya kulingana na umbali uliopo kama kilomita 85.

"Nilichoka (baada ya kusubiri sana), ndipo nilipoamua kuandika barua kumuomba Mkurugenzi (DED) anipe usafiri wa kubeba familia yangu ili nikafanye kazi, pia anilipe stahiki zangu zote kwa maana ya malipo. Nikawa nipo kwenye kituo changu cha awali nikisubiri lini mwajiri atakuja kunichukua na kunilipa stahiki zangu.

"Wakati nikisubiri taarifa kutoka kwa Mkurugenzi ambaye ni mwajiri, Septemba 8, 2022 wakati nipo katika kituo changu pasipo kufanya kazi yoyote, ndipo nilipokea wito katika Ofisi ya Mwalimu Mkuu na baada ya kufika, alinipa taarifa aliyotoka nayo kwenye kikao cha kazi.

"Ni agizo la Ofisa Elimu Wilaya kwamba walimu ambao waliohamishwa vituo, lakini bado wanasubiri stahiki zao, kimsingi kule waliko hawafanyi kazi, lakini hata kituo cha cha awali hawafanyi kazi wakisubiri stahiki zao.

Wapewe vipindi katika vituo vyao vya awali waendelee kufanya kazi.

"Basi nilipewa vipindi nikaanza kufanya kazi Septemba 9, 2022. Nimefanya kazi mpaka Januari 9, 2023 tena nikapata zuio kutoka kwa Ofisa Elimu Kata na Mwalimu Mkuu kwamba wameagizwa na Ofisa Elimu (DEO) kwamba yule mwalimu (mimi) aende kwenye kituo chake alichohamishiwa.

"Mimi sikukataa, niliwambia kwamba nadhani barua yangu bado ipo niliyojibiwa kuwa niendelee kusubiri nikiwa kituo changu cha awali, hatimaye mkanipa tena vipindi. Basi kwa kuwa sijatimiziwa chochote sijapewa stahiki zangu wala usafiri, basi mimi narudi nyumbani nitamkumbusha mwajiri wangu atimize stahiki zangu.



Baraka Mbugi ni Mwalimu Mkuu Shule ya Mpembe.

"Nikaandika barua Januari 13, 2023 (siku nne baadaye) ya kumuomba mwajiri wangu (DED) kama bado bajeti haijaruhusu, aniache katika kituo changu hiki hiki cha awali, lakini mpaka leo sijapata jibu la barua ile," anasimulia mkasa na kuendelea:

"Sikuchoka, nikaenda kwa Ofisa Utumishi nikakaa nae nikamweleza jinsi ninavyonyanyasika.

Alimuita Ofisa Elimu, akaulizwa kuhusu mimi, akasema 'mwalimu huyu anadai stahiki zake za uhamisho'. Ofisa Utumishi akamwambia mwalimu yuko sahihi, inatakiwa apewe stahiki zake ahamishwe, kwa maana ya kupewa usafiri, basi Ofisa Utumishi akaagiza fanyeni juu chini, mafuta yapatikane ahamishwe na alipwe.

"Baada ya hapo ilitokea sintofahamu, ikaonekana kwamba nilishalipwa stahiki zangu. Ndipo tulipoenda kwa mhasibu na kujiridhisha juu ya malipo hayo ambayo Ofisa Elimu alitamka bayana kwamba nilishalipwa.

Baada ya kufika kwa Mhasibu kujiridhisha, wote Ofisa Elimu na mimi, ikaonekana sijalipwa hata shilingi kumi.

"Aliyekuwa anahusika na malipo ni Ofisa Takwimu. Basi siku hiyo hakuwapo, ndipo maajabu ambayo yalinichanganya, Ofisa Elimu wangu akaniambia nichukue namba ya yule Ofisa Takwimu nimpigie simu, nimuombe ile pesa.

Kwa kweli, sikuelewa maana ile ni ofisi, leo mimi nimpigie simu kama vile nilimkopesha ile pesa, kwa kweli, hilo sikuliafiki!

"Mimi nilimwambia ofisa wangu (DEO) kwamba mimi narudi utakapokamilisha taratibu, mimi napatikana palepale kituo changu cha awali, nikawa nimerudi," anasimulia Mwalimu Ndebile kwa hisia ya kulalamika, akinena baada ya wiki mbili kupita tangu afuatilie haki hiyo, akashangaa ghafla mshahara wake umefungwa.

Anaendeleza simulizi ya mkasa: "Baada ya kutopata mshahara wangu wa mwisho wa mwezi Januari (2023), ikabidi niende ofisini (kwenye halmashauri) nikahoji, lakini shinikizo ni lilelile niende kituoni nikafanye kazi na mimi nikawambia siwezi kwenda kituoni wakati stahiki zangu hamjanipa.

"Sikuchoka, Febuari 21 (2023) nikaandika tena barua kwa Mkurugenzi (DED) nikihoji sababu za kunifungia mshahara wa Januari na Febuari...kwanini wamefunga mshahara pasipo kunipa taarifa na kuamua kuchukua maamuzi kama hayo?...

"Kwa kifupi, nanyanyasika, maana hata barua hiyo ya kuomba sababu ya kufungiwa mshahara mpaka dakika hii (Mwezi Aprili) bado haijajibiwa na cha ajabu tena, Machi 3 (23) nikapata shitaka kwamba nashitakiwa na Tume ya Walimu kwamba mimi ni mtoro kazini kwa muda wa siku 210. "Nilizidi kushangaa zaidi, mimi kama mwalimu tunayo mihula miwili kwa mwaka ya masomo na ndani ya mihula hiyo siku za masomo, huwa hazizidi siku 195 (ambazo ni kwa Mujibu wa Sera ya Elimu), sasa leo ni mtoro kwa siku 210.

"Kingine, sheria inaelekeza mtumishi wa umma asipokuwapo kazini ndani ya siku tano pasipo ruhusa, anachukuliwa hatua za kinidhamu.

Sasa leo nina siku 210, nakuja chukuliwa hatua wakati sheria inasema siku tano, kwakweli nanyanyasika naonewa," analalamika Mwalimu Ndebile, akionyesha simanzi.

INAENDELEA UK. 8



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Tanganyika. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

# Simulizi ya mateso mwalimu aliyezuiwa mishahara, kisa kudai haki za uhamisho

INATOKA UK. 7

**MWALIMU MKUU**

Baraka Mbugi ni Mwalimu Mkuu Shule ya Mpembe, anakiri Mwalimu Ndebile Malcom, alikuwa shuleni hapo tangu mwaka 2010, kabla ya kupata uhamisho mwaka 2022 kwenda Shule ya Msingi Mwikang'ombe, akaenda kuripoti kwenye kituo kipya cha kazi kwa miezi sita na kukutana magumu ya kushindwa kuhamisha familia na vifaa vyake, hata akaandika barua kuomba arudi kituo chake cha awali, wakati anasubiri stahiki za uhamisho.

Pia, Mwalimu Mkuu anakiri kupata maelekezo ya Ofisa Elimu Wilaya kumtaka ampangie vipindi Mwalimu Ndebile, wakati anaendelea kufuatilia stahiki zake, kabaki anafundisha shuleni Mpembe kati ya Septemba mwaka jana na Januari mwaka huu.

Kuhusu kilichofuata, Mwalimu Mkuu anaeleza:"Niliitwa ofisini nikaambiwa huyo mwalimu anatakiwa arudi kule kwenye kituo chake cha Mwikang'ombe. Kweli mwalimu nilimwambia, lakini sasa stahiki zake za uhamisho alikuwa hajapata.

Alivyoenda kule (ofisi halmashauri) wamejibizana na mwajiri wake pamoja na Ofisa Elimu, mpaka sasa yupo hapa bado hajaenda kule akiwa anasubiri stahiki zake.

"Ameshasimamishiwa mshahara na yupo kwenye hatua za kuomba wamfungulie mshahara. Sijajua mpaka sasa kama amefanikiwa, maana kwa sasa hayupo kwenye kituo chake, sijajua kwa mwezi huu (Aprili)..." anasema Mkuu wa shule Mbugi.

**MKURUGENZI TANGANYIKA**

Nipashe lilimtafuta Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Tanganyika, Shaban Juma, kufafanua mkasa huo, naye akakana kulijua, akitamka: "Huyo Mwalimu ni mwalimu gani? Inatakiwa taarifa zake zije hapa, ili tuzione hizo data zinazosema alikwenda kuripoti akafanya kazi miezi sita mpaka sasa hajalipwa stahiki zake, sina taarifa hizo.

"Maana kuna walimu mpaka sasa mashitaka yao yanashugulikiwa, isije kuwa ni miongoni mwa hao na huenda ikawa tayari taarifa zake zishatolewa. Sababu nilishapokea idadi ya walimu ambao tayari mashitaka yao yamekwenda kwenye Kamati ya Nidhamu na yamesikilizwa na wengine wamefukuzwa, wengine wamepewa maonyo na tayari yamekuja katika meza yangu.

"Kama kuna mwalimu ambaye ana malalamiko yoyote, inatakiwa aje katika ofisi yangu ashughulikiwe. Ofisi ya Mkurugenzi ndio inaweza kushughulikia matatizo yote ya watumishi. Hivyo, inatakiwa huyo mwalimu aje hapa, kama alisharipoti akafanya kazi miezi sita bado ana tatizo, hilo basi hilo ni suala jingine.

"Inatakiwa aje tuliangalie hilo suala tuone na hilo faili lake tuliangalie, ili tulishughulikie kwa pamoja na Ofisa Elimu na mamlaka zingine, tuhakikishe kama ana stahiki zake zinazotakiwa kulipwa alipwe maisha mengine yaendelee,"

Kuhusu kufungia mishahara, anasema:"Mtumishi anapofungiwa mshahara ina maana hafiki katika kituo chake cha kazi, ni lazima afike katika kituo chake cha kazi kama kahamishwa basi afike kwenye kituo anachotakiwa kwenda kuripoti na awe yupo kazini, ili taratibu zingine ziendelee.



Asteria Mfulungu, mke wa Mwalimu Ndebile akizungumza nyumbani.

"Tunao walimu wengi ambao wengine wapo tu mtaani wanarandaranda na sasa hivi wengine wamesimamishiwa mshahara.

Hilo tatizo limetokana na utovu wa nidhamu, ambao umeanza kujitokeza kwa baadhi ya watumishi hasa walimu, ambao wamekuwa hawafiki katika maeneo ya kazi, wanakuwa wapo mjini, baadae wanapotafutwa hawaonekani.

"Lazima tusimamishe mshahara wao ili waje. Wanapokuja, tuendelee na matatizo mengine ya kinidhamu ambayo yanatakiwa yashughulikiwe ili maisha mengine yaendelee, kwa sababu kila mtu ameajiriwa ili kutoa huduma kwa wananchi," anatamka Mkurugenzi, anayekiri ndani ya miezi sita sasa, washapokea fedha na kuwalipa wadai stahiki za uhamisho.

**MAISHA YA MWALIMU**

Nipashe ikamtembelea mwalimu kupata uhalisia wa maisha yake kwenye makazi anakoishi, ikimkuta Mwalimu Ndebile, anasema tayari kukosa mshahara kumemuathiri kwa mengi ya msingi kifamilia.

"Najiuliza hii familia nitaiendeshaje bila mshahara? Nina watoto wako shule wananitegemea na mimi nategemea kazi yangu hii, nashindwa kuelewa hatima yake itakuwaje ikiwa leo nina mwezi wa pili, pia nina shitaka ambalo natakiwa nilijibu ndani ya siku 15, bado mshahara wa mwezi wa Tatu, pia sitopata, familia inaendelea kupata madhara.



Mwalimu Ndebile Malcom, akizungumza nyumbani kwake. **PICHA ZOTE: NEEMA HUSSEIN.**

"Serikali naiomba inisaidie sasa nipate stahiki zangu, mimi sijakataa uhamisho, uhamisho upo kwa mujibu wa sheria kwamba mtumishi yeyote wa serikali anapaswa ahame, ili kurekebisa upungufu wa wafanyakazi katika kituo husika.

"Naiomba serikali pia inihakikishie, maana hii tayari inaleta sitofahamu na inakuwa ni shida baina ya mimi na mwajiri wangu, kama alitoa ridhaa ya kuendelea kufundisha na baadae akanisimamisha tena, nakuwa na hofu kwamba hapo baadaye itakuwaje, kwa hiyo kwa lolote lile wanaweza kunifanyia, maana wao ndio viongozi.....," analalamika

Asteria Mfulungu, mke wa Mwalimu Ndebile, anasema mara baada ya mumewe kufungiwa mshahara, maisha yao yamekuwa magumu, kwani mumewe hana kazi nyingine na muda waliotumia kufunga mshahara, umekuwa kipindi kigumu kwao, ambacho hata vyakula havijakomaa mashambani.

Juzi Jumamosi, Nipashe iliwasiliana Mwalimu Ndebile, anasema Chama cha Walimu kimefungua kesi ya dharura kumtentea dhidi ya Mkurugenzi wa Tanganyika na mahakama imeamuru alipe mshahara na kuhoji kulikoni dai la kutohudhuria kazini siku 210. Anakiri kupokea mshahara wa Aprili, huku hajapata malipo yake ya miezi mitatu, na pesa za uhamisho.

**SHERIA INAVYOSEMA**

Kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazi, 2004, ina maangalizo yafuatayo:

Sura ya Sita ya Sheria inatamka: "Kazi ya lazima, inajumuisha kazi ya utumwa au kazi yoyote iliyolazimishwa kwa mtu kwa vitisho vya adhabu na ambayo mtu huyo hajaridhika." Pia kifungu chake, kinatoa ufafanuzi "kazi yoyote inayotolewa katika hali ya hatari au mazingira ambayo yatahatarisha uwepo au maisha mazuri ya jamiiyote au sehemu ya jamii"

Vilevile, Sura ya Saba inanena "Kila mwajiri atatakiwa kuhakikisha kwamba anaendeleza fursa sawa katika ajira na kujitahidi kuondoa 'ubaguzi' katika sera yoyote ya ajira mazoezi kwa vitendo." Pia inafafanuliwa "kudhalilishwa kwa mfanyakazi kutakuwa ni aina ya ubaguzi na kunatakiwa kuzuiwa na mtu yeyote, au kwa ujumla...,"

Inaendelezwa katika Sura ya Nane kwamba: "Kama mfanyakazi ataweza kujenga kesi iliyothibitishwa ya 'ubaguzi' wa mwajiri kwa sababu yoyote iliyotajwa... itakuwa ni wajibu wa mwajiri kuthibitisha..."

Sura ya 28 usalama wa malipo, ina angalizo "Mwajiri hatakiwi kufanya makato yoyote kutoka kwenye ujira wa mfanyakazi, labda makato yanatakiwa au yanaruhusiwa chini ya sheria iliyoandikwa, mkataba wa hiari, upangaji wa mishahara, amri ya mahakama au tuzo ya usuluhishi; au inatajwa mwajiri awe amempa mfanyakazi kwa maandishi, chanzo, kiasi na mahesabu ya makato."

# Mbunge ahamasisha walimu kujadili athari tabianchi

**Na Tumaini Mafie,** MONDULI

MBUNGE wa Monduli (CCM), mkoani Arusha, Freddy Lowassa, ameanza kutekeleza kampeni yake ya kuhamasisha walimu wa shule za msingi na sekondari wilayani humo, kujadili athari za mabadiliko ya tabianchi na wanafunzi wao ili kizazi kijacho kiweze kukabiliana na athari hizo.

Lowassa, alitangaza juzi kuanza kwa kampeni hiyo, wakati aliposhiriki mahafali ya 57 Chuo cha Ualimu Monduli, ambako alishuhudia wahitimu 400 wakihitimu mafunzo ya Stashahada ya Elimu ya Sekondari na Astashada ya Elimu ya Msingi.

"Nendeni mkafundishe athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu kumekuwapo na athari mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi, hususani katika wilaya yetu ya Monduli. Mnakumbuka mabadiliko hayo yalisababisha mwaka jana, mamia kwa makumi ya mifugo kupoteza maisha kutokana na ukame uliotokana na ukame.

"Ninyi mkiwa kama walimu, ni vizuri mkatumia muda wenu mwingi kujadili masuala hayo darasani na nje ya darasa na kuweka mikakati ya kupambana na ukame.

"Nimefurahi sana kuona chuo hiki mmeotesha miti zaidi ya 6,000; ni jambo zuri sana kwa sababu limesaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, naomba muendelee na utaratibu huu, kwa kuwa unasaidia Wilaya ya Monduli kuendelea kuwa ya kijani."

Aliwahimiza wahitimu hao kuitumia elimu waliyoipata kuleta mabadiliko katika jamii na kuwa mfano wa kuigwa, kwa kuwa ualimu ni taaluma na wito na inapaswa kuheshimiwa na kila mtu.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Samwel Irira, alisema kwa sasa chuo hicho kina wanafunzi 1,087, huku hali ya taaluma ikiwa ni nzuri kutokana na kuwaandaa walimu hao kuajiriwa na kujiajiri wenyewe.

"Pamoja na mafanikio hayo, ni ukweli usiopingika kwamba bado tunakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo kukosekana kwa jengo la utawala, nyumba za wafanyakazi ni chakavu, lakini udogo wa jengo la maktaba, hauendani na idadi ya wanachuo walioko, pamoja na kukosekana maabara ya masomo ya sayansi," alisema Prof. Irira.

Kwa mujibu wa Prof. Irira, tatizo jingine ni uhaba wa matangi ya maji, kwa kuwa yaliyoko ni machache kulingana na idadi kubwa ya wanafunzi ilionao.

Akijibu hoja ya upungufu wa matangi ya maji, Mbunge Lowassa aliahidi kutatua tatizo hilo kupitia fedha za Mfuko wa Jimbo katika mwaka ujao wa fedha 2023/24.

# Kushuka thamani ya Euro kwaathiri mradi nishati jua

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUSHUKA kwa thamani ya fedha ya Umoja wa Ulaya (Euro), kutokana na vita vya Urusi na Ukraine, kumeathiri bajeti ya utekelezaji mradi wa uimarishaji umuhimu wa nishati ya jua katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji, kwa ajili ya kupunguza umaskini kwa wananchi karibu na Mlima Kilimanjaro.

Aidha, mfumuko wa bei kwa bidhaa za ujenzi na solar katika kipindi cha mwaka 2022, pamoja na matokeo ya utafiti wa upatikanaji wa maji katika eneo hilo, zimeongeza kina cha uchimbaji wa visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kubadili makadirio na gharama za uchimbaji wake.

Akitoa taarifa kwa wadau wa mradi huo mwishoni mwa wiki kuhusu utekelezaji wake, Mratibu wa Utafiti, Sera na Ubunifu kutoka Shirika la CAN Tanzania (Climate Action Network Tanzania), Mkombozi Mbekenga, alisema licha ya kuwapo kwa matatizo hayo, bado mradi huo ni fursa kubwa kwa wakulima wa Kijiji cha Kilimambogo, Ngosero na Mkombozi vilivyoko Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, ambao wanafikiwa na maji hayo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. 187,135,282, unaofadhiliwa na Serikali ya Ujerumani, kupitia Shirika la GIZ, kwa kipindi cha miezi 18; una dhana ya kushawishi matumizi ya nishati jadidifu katika kuwezesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji; kwa kuwa matumizi ya nishati hiyo, yanalenga kwenye uchangiaji wa malengo ya kitaifa na kimataifa yenye maono ya kupunguza uchafuzi wa hali ya anga na kutunza mazingira.

Kwa mujibu wa CAN Tanzania, mpaka kufikia sasa visima viwili vimekamilika, Kijiji cha Mkombozi kina urefu wa mita 130 na cha Kijiji cha Kilimambogo kina urefu wa mita 80.

"Baada ya kumalizika shughuli za uchimbaji, kujenga minara na kuweka mapipa, CAN Tanzania, ilitangaza zabuni ya kufunga mitambo ya kuvuta maji kwa kutumia nishati ya jua, Kampuni ya Ag Energies ilishinda zabuni hiyo na imefunga mtambo wa kuvuta maji katika Kijiji cha Mkombozi wenye paneli 34 zenye jumla ya wati 11,050 na pampu yenye nguvu ya farasi 10.

"Wakati katika Kijiji cha Kilimambogo, kumefungwa mtambo wenye paneli 34 kama ilivyo kwa Mkombozi na pampu yenye nguvu ya farasi 7.5. Katika Kijiji cha Ngosero, bwawa moja lenye uwezo wa kubeba lita milioni 10, limejengwa na kukamilika na hadi sasa limekusanya maji ya mvua za vuli na mvua za masika."

Akizungumzia mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Dionis Myinga, alisema CAN Tanzania wamekuja na miradi ya umwagiliaji, ambayo ni lengo mahususi la serikali kuhakikisha wananchi wake wanafikia azma yao ya kujitegemea kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali na utunzaji mazingira.

"Kimsingi miradi hii imeshatekelezwa katika maeneo ya wanufaika waliolengwa kwenye Kata za Masama Kusini na Kata ya Weruweru. Miradi hii kweli inatekelezwa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi wa Wilaya ya Hai na taifa kwa ujumla.

Tuwaombe waendelee kutazama na maeneo yetu mengine kunufaika na miradi hii," alisema.



Diwani wa Kata ya Mbaramo wilayani Muheza mkoani Tanga, Pugae Mohamed akizungumza katika Kituo cha Afya cha Ubwari mbele ya Mkuu wa wilaya ya Muheza, Juma Irando (Wapili kulia) baada ya kusikitishwa na vitendo vya mmomonyoko wa maadili nchini ikiwamo ushoga na ndoa za jinsia moja huku akiwataka wazazi kuwalinda watoto wao wa kiume wakati bado wadogo. Kulia ni Katibu Tawala wilaya hiyo, Desderia Haule na Wapili kushoto ni Mganga mkuu wilaya hiyo Frola Kessy. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Waganga tiba asili, wahubiri injili waonywa kung'ang'ania wagonjwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WIZARA ya Afya, imewaonya waganga wa tiba asili pamoja na wahubiri wa injili, kuacha kung'ang'ania wagonjwa wanaofika kwao wakiwa hoi, badala yake wanaostahili wapatiwe rufani haraka ya kwenda kupata huduma zaidi za tiba, uchunguzi na matibabu ya kibingwa kwenye hospitali kubwa za umma.

Ofisa Programu ya Uelimishaji, Uhamasishaji na Ushirikishwaji Jamii wa Wizara hiyo, Magdalena Dinawi, alitoa hari hiyo mwishoni mwa wiki, wakati akizungumza na wajumbe wa kamati ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko na mengine katika Wilaya ya Babati, mkoani Manyara. "Wagonjwa wanaowafikia ili wawahudumie, wasiwa-ng'ang'anie na kuwaacha waendelee kuugua. Lakini pia, waganga wa tiba asili ukipiga ramli ukashindwa, tuletee wagonjwa hao; waambie nenda kwenye yale majengo ya hospitali ili mpate vipimo zaidi," alisema Dinawi.

Dinawi, alisema uamuzi wa wizara hiyo kuanza kupita mikoani na wilayani kutoa elimu hiyo ni kuwezesha kufikisha elimu kwa umma kwa magonjwa ya mlipuko.


Aidha, hivi sasa wizara hiyo inawaelekeza hivyo, kwa kuwa kuna magonjwa ya kuambukiza, ambayo watu wa tiba asili na viongozi wa dini hawayawezi.

Alisema japo viongozi wa dini wamepewa neema ya kuombea mapepo yatoke, wasijipe jukumu la kutoa mapepo kwenye magonjwa ya mlipuko, badala yake waache jukumu hilo kwa wataalamu wa afya.

Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Twange, alisema afya ndiyo mtaji wa kwanza kwa binadamu. Huku akiwashukuru viongozi wa dini kwa kuwasaidia kuwapa nafasi ya kutoa elimu kanisani na misikitini.

Awali, Mkuu wa Divisheni ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Dk. Kyabaroti Peter, alisema suala la kujikinga linahitaji ushirikishwaji wa wadau wengi.

Mchungaji Kiongozi wa Usharika wa Babati wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jasson Kahembe, alisema milango iko wazi Wizara ya Afya kupeleka wataalamu wake kwenye ngazi za kata na vjiji ili watoe elimu pia kanisani.





## JUAKITA kukabiliana ndoa jinsia moja

**Na Waandishi** WETU

UMOJA wa Wanawake wa Dini ya Kiislamu (JUAKITA), wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameanza mpango wa kulaani na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo, ushoga, usagaji na mapenzi ya jinsia moja vinavyofanywa na baadhi ya watu wasiokuwa na hofu ya Mungu na kuharibu taswira njema ya utamaduni wa Mtanzania.

Mwenyekiti wa umoja huo, Bahati Mrisho, aliyabainisha hayo hivi karibuni wakati akizungumza na wanawake wa umoja huo katika Msikiti Mkuu wa Ijumaa wa Masjid Nuru na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Shekhe Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka.

Alisema, watoto na vijana wa kubalehe wanaharibika kwa kukosa malezi mazuri ya wazazi, kila mlezi anatakiwa kuwa mstari wa mbele kutoa malezi bora ili kuwanusuru na mmomonyoko wa maadili wa kujiingiza katika vitendo vya ushoga, usagaji na mapenzi ya jinsia moja ambayo yameendelea kuenea kwa kasi katika jamii. Naye Shekhe wa Wilaya ya Kahama, Alhaji Omary Damka, alisema suala la maadili halibagui madhehebu wala kabila hivyo kila mmoja ana wajibu wa kulikemea kwa imani yake na kuwataka kinamama wanapoona nyumba mitaani haieleweki inaingiza vijana wa kiume na kike watoe taarifa kwa viongozi walio jirani yao.

Kadhalika, mkoani Mara jamii imetakiwa kulaani vitendo vya ushoga na ulawiti kwa kuwa hata maandiko matakatifu yanalaani vikali vitendo hivyo.

Hayo yalibainishwa juzi na Mbunge wa Jimbo la Tarime, Michael Kembaki, wakati akitoa vifaa tiba mbalimbali ikiwamo X-ray, msaada uliotolewa na wahisani, Human Branch, kutoka Sweden vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.5 katika Hospitali ya Bomani. Alisema kuna haja ya jamii kuendelea kukemea na kulaani vikali wimbi la ushoga, ulawiti na ndoa ya jinsia moja, vitendo vinavyoikumba dunia na serikali pekee haiwezi kudhibiti vitendo hivyo bila ya ushirikiano wa jamii.

*Imeandaliwa na Shaban Njia (KAHAMA) na Timothy Itembe (TARIME).

# Maji Ziwa Victoria kunufaisha wananchi 2,000 Kishapu

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI 2,000 wa vijiji vya Bupigi na Butungwa wilayani Kishapu, wameondokana na matumizi ya maji machafu, baada ya kuzinduliwa mradi mkubwa wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria.

Akizindua mradi huo juzi, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Christina Mndeme, alisema mradi huo kutoka Ziwa Victoria katika kijiji cha Bupigi wilayani Kishapu, utanufaisha pia na wananchi wa Kijiji cha Butungwa.

Alisema wananchi wa vijiji hivyo viwili vya Bupigi na Butungwa wataondokana na matumizi ya maji machafu yakiwamo ya mito, visima na mabwawa, na kutumia majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria, huku akiwataka waitunze miundombinu ya mradi huo ili uwahudumie kwa muda mrefu bila ya kuharibika.

"Kabla ya Muungano wananchi wengi mlikuwa mkitumia maji ya kwenye mabwawa, visima na mito, lakini baada ya Muungano wananchi mnatumia majisafi na salama yakiwamo kutoka Ziwa Victoria hadi huku maeneo ya vijijini," alisema Mndeme.

Aidha, aliwaagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani Kishapu kuhakikisha wanaongeza vituo vingi vya kuchotea maji, ili wananchi hasa kinamama wasipate tabu ya kutembea tena umbali mrefu kuyafuata. Baadhi ya wanawake wa Bupigi wilayani Kishapu, akiwamo Regina Maduka, walipongeza serikali chini ya Rais Samia kwa kuwatekelezea mradi huo, ambao umewaondolea adha ya kutumia maji machafu na kutopoteza muda wa kufuata umbali mrefu.

Meneja RUWASA wilayani Kishapu, Mhandisi Dickson Kamanzima, alisema mradi huo wa maji Bupigi na Butungwa utanufaisha wananchi 2,000 na ulianza kutekelezwa mwaka jana na umegharimu Sh. milioni 499.5.




Baadhi ya vijana wa dini ya kiislamu wanaosoma elimu ya dini hiyo misikiti mbalimbali wakiwa wameshikilia bango lenye ujumbe wa kulaani vikali ndoa za jinsia moja, ushoga, usagaji na ubasha wakati wa maandamano ya Amani ya kupiga vitendo hivyo yaliyoongozwa na Shekhe wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga Alhaji Omary Damka, juzi.**PICHA: SHABAN NJIA.**

# Chalamila aagiza uwekwaji taa za barabarani

**Na Titus Mwombeki,** KYERWA

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo kusimamia wakandarasi waliofanya makubaliano ya kuweka taa za barabarani katika maeneo mahususi mkoani humo waziweke haraka kama makubaliano ya mkataba yalivyo ili kuondoa adha wanazokumbana nazo watumiaji wa barabara hizo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa ziara yake katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, wakati wa ukaguzi wa mradi wa barabara ya utawala yenye urefu wa kilomita 1.2, ambayo imekamilika kwa asilimia 90 na kugharimu Sh. milioni 500.

"Nimeridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kutokana na kuwa na uhalisia wa kazi zilizofanyika na fedha iliyotolewa na serikali niwatake wakurugenzi wote mhakikishe mnasimamia hili suala la kuweka taa ziwekwe kwa wakati," alisema Chalamila.

Meneja Wakala wa Barabara Mijini wa Vijijini (TARURA) wa Wilaya ya Kyerwa, Yetron Mbasha, alisema mpaka sasa ujenzi wa barabara hiyo umekamilika kwa asilimia 90 na bado kuweka taa zilizoletwa na mkandarasi tofauti na aliyekuwa akijenga.

"Kulingana na asili ya eneo hili ya mbolea na uoevu uliopo tumekata hadi sentimita 50 mpaka 60 ambapo kazi ya kwanza tulianza kukata sentimita 50, kilichobaki ni kuweka taa na hili limechelewa kutokana na taa zilizoletwa na mkandarasi kuwa tofauti na zilikuwa zimeainishwa katika mkata tulikaa na kuweza kuzikataa na tayari mkandasi ameishaagiza taa lengwa," alisema Mbasha.

Baadhi ya wakazi wa mji wa Rubwera, halmashauri hiyo walisema kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya kilometa 1.2 kwa kiwango cha lami katika maeneo ya utawala itarahisisha shughuli za usafiri kutokana na eneo hilo kuwa korofi wakati wa mvua. "Kutokana na wilaya yetu kuwa changa bado miundombinu yetu ni tatizo, lakini tunaishukuru serikali kwa ujenzi wa barabara hii itasaidia sana sio kwetu wanakyerwa tu bali hata wafanyabiashara ambao wanakuja huku kutoka mikoa ya jirani kuchukua mazao," alisema, Amon Mjini, mkazi wa Kyerwa

Nipashe
# Spotika



WACHEZAJI 10 'WAZEE' WENYE THAMANI ZAIDI UK. 12-13

# WACHEZAJI WA5 WANAOLIPWA ZAIDI LALIGA 2022-23



HAZARD

**MADRID** Hispania

LIGI Kuu ya Hispania, LaLiga inachukuliwa kuwa moja ya ligi bora zaidi duniani. Kwa miaka mingi. Ligi hiyo imekuwa ikivutia na kuhifadhi wachezaji wakubwa zaidi duniani, huku klabu kama Real Madrid na Barcelona zikiwa zinatawala zaidi.

Klabu hizi zimeweza kulipa mishahara mikubwa kwa wachezaji wao kutokana na vyanzo vyake vingi vya mapato, ambavyo vinatokana na vyanzo mbalimbali kama vile mauzo ya tiketi, bidhaa na dili za utangazaji.

Kutokana na hali hiyo, wameweza kuwavutia na kuwabakisha baadhi ya wanasoka bora duniani, na kuifanya LaLiga kuwa miongoni mwa ligi zenye ushindani na kusisimua kuitazama.

Hapa tunaangalia wachezaji watano wanaolipwa fedha nyingi zaidi kwenye LaLiga msimu huu wa 2022-23, twende sasa...

**#5 Vinicius Junior (Real Madrid) – Euro milioni 1.67 kwa mwezi**

Vinicius Junior hapo awali alichukua tahadhari kama winga mahiri wa Brazil ambaye alikuwa amejaa kila aina ya uwezo na angeweza kuwafanya mabeki kukimbia mara kwa mara. Kwa kweli ametumia uwezo wake katika misimu michache iliyopita na amefanikiwa kuwa mmoja wa washambuliaji bora zaidi kwenye sayari hii.

Katika mechi 42 kwenye michuano yote akiwa na 'Los Blancos' hadi sasa msimu huu, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, amefunga mabao 19 na kutoa asisti 13. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaonekana kuwa tayari kuongoza mashambulizi ya Real Madrid kwa siku zijazo. Ni mmoja wa wachezaji wanaolipwa zaidi LaLiga na anapokea Euro milioni 1.67 kwa mwezi.

**#4 David Alaba (Real Madrid) – Euro milioni 1.88 kwa mwezi**

Kuondoka kwa David Alaba kutoka Bayern Munich kuliashiria mwisho wa kipindi cha mafanikio cha miaka 11 akiwa na timu hiyo ya Baravia ambapo alishinda mataji 27 makubwa. Alijiunga na Real Madrid kwa mkataba wa miaka mitano kama mchezaji huru, na kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika timu na kuongeza uzoefu muhimu na ustadi kwenye kikosi.

Alaba alionyesha kiwango chake na uzoefu katika msimu wake wa kwanza katika mji mkuu wa Hispania, akicheza jukumu muhimu katika ushindi wao wa LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Yeye ni mwanasoka hodari ambaye anaweza kucheza katika nafasi nyingi.

Gwiji huyo wa Austria anaingiza Euro milioni 1.88 kwa mwezi, na kumfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi LaLiga.

**#3 Sergio Busquets (Barcelona) – Euro milioni 1.91 kwa mwezi**

Sergio Busquets ni mmoja wa viungo wakubwa wa zama za kisasa. Amekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya Barcelona na Hispania kwa miaka mingi.

Amemudu vema nafasi ya kiungo mkabaji na uwezo wake wa kuusoma mchezo na kuvunja mashambulizi ya wapinzani umekuwa muhimu kwa wababe hao wa LaLiga.

Akili na utulivu wa Busquets kwenye mpira pia umemruhusu kuanzisha hatua za kushambulia na kuweka kasi ya mchezo, na kumfanya kuwa mchezaji muhimu kwa klabu na nchi. Kwa sasa yuko katika mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Barca na kuna uwezekano mkubwa wa kusaini mkataba mpya katika klabu hiyo.

Busquets huweka mfukoni Euro milioni 1.91 kwa mwezi kutokana na mkataba aliosaini mwaka 2018.

**#2 Robert Lewandowski (Barcelona) – Euro milioni 2.17 kwa mwezi**

Robert Lewandowski ni mfungaji mabao wa ajabu ambaye ametoa nguvu katika kipindi cha kazi yake ya kifahari. Uwezo wake bora wa kufunga mabao ulimsaidia kupata tuzo za Kiatu cha Dhahabu cha Ulaya katika misimu ya 2020-21 na 2021-22.

Lewandowski aliondoka Bayern Munich msimu uliopita na kujiunga na Barcelona. Wakatalunya hao walikuwa wakihitaji sana mshambuliaji wa kutegemewa na walichukua nafasi hiyo kumsajili mshambuliaji huyo mashuhuri wa Poland.

Walimfunga kwa mkataba mnono ambao ulimfanya kuwa mmoja wa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi LaLiga. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, anapokea mshahara wa euro milioni 2.17 kwa mwezi.

**#1 Eden Hazard (Real Madrid) – Euro milioni 2.25 kwa mwezi**

Katika msimu wa majira ya joto wa 2019, Real Madrid ilimsajili Eden Hazard kutoka Chelsea kwa rekodi ya klabu ya Euro milioni 115. Matarajio yalikuwa makubwa kwa winga huyo wa Ubelgiji, lakini majeraha na hali duni hivi punde vilikatiza muda wake katika klabu hiyo.

Hazard alijitahidi kuiga kiwango alichoonyesha akiwa Chelsea na kushuka kwake kulikuwa kwa kasi huku akikosa mechi nyingi kutokana na majeraha mbalimbali. Licha ya kuwa na kipaji, Hazard kwa kiasi kikubwa amekuwa akiwakatisha tamaa Real Madrid na hatma yake katika klabu hiyo bado haijafahamika.

Amecheza jumla ya mechi nane katika mashindano yote akiwa na Real Madrid msimu huu, lakini bado anaingiza mshahara wa Euro milioni 2.25 kwa mwezi.

## ISIKUPITE

KARIM Benzema amekuwa mchezaji wa pili katika historia ya Real Madrid kufunga mabao 350 kwa klabu hiyo baada ya Cristiano Ronaldo ambaye ni mchezaji pekee aliyeifungia zaidi ya mabao hayo [451] kabla ya kuondoka klabuni hapo mwaka 2018. Aidha, Benzema yupo katika mbio nzuri za kutwaa 'Pichichi' [Tuzo Mfungaji Bora LaLiga] kutokana na kufikisha mabao 17, moja nyuma ya Robert Lewandowski wa Barca.



## Extra Time



DE BRUYNE

# WACHEZAJI 10 'WAZEE' WENYE THAMANI ZAIDI

**LONDON,** England

UTHAMANI wa wachezaji wa soka kwenye soko la uhamisho huamuliwa na mambo mbalimbali kama vile umri wa mchezaji, urefu wa mkataba, kiwango cha wakati huo na uwezekano wa kuendelezwa siku zijazo.

**Timu pia huzingatia nafasi ya mchezaji, malengo, pasi za mabao na vipimo vingine vya uchezaji, pamoja na sifa na soko la mchezaji. Ada za uhamisho zinaweza kuathiriwa na historia ya uhamisho wa mchezaji, hali ya soko la wakati huo la uhamisho, na uthabiti na udharura wa kifedha wa klabu ya ununuzi na uuzaji.**

Hatimaye, thamani ya soko ya uhamisho ya mchezaji wa soka inategemea mazungumzo na inaathiriwa na thamani inayoonekana ambayo kila klabu inaweka kwa mchezaji. Wachezaji wanapovuka miaka 30, thamani yao kawaida hushuka.

Lakini kuna watu ambao wanacheza soka bora hata wakiwa na miaka 30 na hawaoneshi dalili zozote za kupungua, hawa hapa...

### #10 Riyad Mahrez (Manchester City) – Euro Mil. 30

Umaridadi wa Riyad Mahrez umemfanya avutiwe na watu wengi kote duniani. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Algeria ni mmoja wa mawinga bora zaidi duniani na ana uwezo mkubwa na akili ya mchezo.

Mshambulizi huyo wa Manchester City amefunga mabao 10 na kutoa pasi nne za mabao katika mechi 26 kwenye michuano yote hadi sasa. Ana umri wa miaka 31, na kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 30.

### #9 N'Golo Kante (Chelsea) – Euro Mil. 30

Haikuwa muda mrefu uliopita ambapo N'Golo Kante alizingatiwa sana kama mmoja wa wanasoka bora kwenye sayari. Ni mmoja wa viungo bora wa ulinzi wa zama za kisasa na amepata mafanikio mengi katika ngazi ya klabu na kimataifa, akishinda Kombe la Dunia mwaka 2018 na Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Chelsea mwaka 2021.

Lakini Kante mwenye umri wa miaka 32, amekuwa akikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara ya hivi karibuni. Kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 30.

### #8 Karim Benzema (Real Madrid) – Euro Mil. 35

Karim Benzema alishinda Ballon d'Or mwaka 2022 baada ya kuwa na msimu bora zaidi wa maisha yake akiwa na umri wa miaka 34. Bado anaendelea vema akiwa na umri wa miaka 35 kwa sasa na ana msimu mzuri sana kwa Real Madrid.

Mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Ufaransa, amefunga mabao 17 kwenye LaLiga msimu huu akiwa na Los Blancos. Ana thamani ya soko la uhamisho ya euro milioni 35.

### #7 Kalidou Koulibaly (Chelsea) – Euro Mil. 35

Chelsea ilimsajili Kalidou Koulibaly msimu uliopita wa majira ya joto kwa euro milioni 38. Beki huyo wa kati wa zamani wa Napoli, anatazamwa na wengi kama mmoja wa mabeki bora wa kati wa kizazi chake. Hajafurahia mwanzo mzuri wa maisha akiwa Chelsea. Thamani ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ni Euro milioni 35.

### #6 Jorginho (Arsenal) – Euro Mil. 35

Jorginho alijiunga na Arsenal mwezi uliopita kwa dau la Euro milioni 11.3. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia ni kiungo anayeshikilia nafasi ya juu, lakini hajakuwa katika kiwango bora msimu wa 2022-23. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, atakuwa na matumaini ya kufufua soka lake Arsenal.

Jorginho kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 35. Kwa hiyo, inaonekana kama 'Washikabunduki' wangejipatia dili kubwa ikiwa Jorginho anaweza kurejea kwenye viwango alivyoonyesha misimu michache iliyopita, itakuwa tamu zaidi.

### #5 Robert Lewandowski (Barcelona) – Euro Mil. 45

Barcelona walilipa euro milioni 45 kumnunua Robert Lewandowski msimu uliopita wa majira ya joto. Ulikuwa uamuzi mzuri kwa Wakatalunya hao kwani Lewandowski amekuwa hodari mbele ya lango msimu huu. Kiwango chake kimechangia kwa kiasi kikubwa kuwafanya wapokee pointi nane kileleni mwa jedwali la LaLiga.

Lewandowski mwenye umri wa miaka 34, amefunga mabao 23 na kutoa pasi tano za mabao katika mechi 25 alizocheza kwenye mashindano yote akiwa na 'Blaugrana' hadi sasa msimu huu.

### #4 Lionel Messi (Paris Saint-Germain) – Euro Mil. 50

Lionel Messi ana umri wa miaka 35 sasa, lakini amecheza soka la kustaajabisha msimu huu. Uzuri wake binafsi uliisaidia Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia na amekuwa katika hali nzuri kule Paris Saint-Germain.

Messi amefunga mabao 15 na kutoa asisti 14 katika mechi 24 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na PSG hadi sasa msimu huu. Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 50.

### #3 Virgil van Dijk (Liverpool) – Euro Mil. 50

Virgil van Dijk amekuwa na mchango mkubwa kwa Liverpool kwenye eneo la ulinzi na amekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio yao chini ya kocha Jurgen Klopp. Beki huyo wa kati wa Uholanzi aliigharimu Liverpool euro milioni 84.65 mwaka 2018.

Van Dijk ana umri wa miaka 31, sasa na anaendelea kuwa mtu wa kutegemewa ingawa uwezo wake unaweza kuwa umepungua kidogo katika kipindi cha mwaka jana. Kwa sasa ana thamani ya Euro milioni 50.

### #2 Neymar Mdogo (Paris Saint-Germain) – Euro Mil. 75

Neymar Jr. amekuwa katika kiwango bora PSG msimu huu. Katika mechi 25 kwenye michuano yote hadi sasa msimu huu, nyota huyo wa Brazil amefunga mabao 17 na kutoa pasi za mabao 15 kwa wachezaji wa Paris.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, ni mmoja wa washambuliaji bora wa karne ya 21 na ni furaha kutazama kila anapopiga mpira. Neymar kwa sasa ana thamani ya euro milioni 75.

### #1 Kevin De Bruyne (Manchester City) – Euro Mil. 80

Kevin De Bruyne ndiye kiungo bora zaidi wa kizazi chake. Sifa za kiufundi za mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji pamoja na maono yake na akili ya mchezo vinamfanya kuwa mmoja wa wachezaji hatari zaidi wa zama hizi.

De Bruyne amekuwa mtu mkuu wa Manchester City chini ya kocha Pep Guardiola. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, amefunga mabao matatu na ametoa pasi nyingi za mabao 17 katika mechi 27 kwenye michuano yote aliyoichezea City kufikia sasa msimu huu. Ana thamani ya Euro milioni 80.

## Nukuu

"Iwapo atarudi Barcelona, itakuwa si kwa mashabiki tu bali kwa wachezaji, kitu cha kushangaza ni kwa sababu nafasi yake ni hapa Barcelona. Sijui nini kinaendelea ... natumai kuwa msimu ujao tunaweza kucheza pamoja kwa sababu najua kuwa Leo ndiye mtu anayeweza kufanya [kutengeneza] kitu bila chochote na bila shaka tunahitaji aina kama hizo za wachezaji, kwa kweli," **mshambuliaji wa Barcelona, Robert Lewandowski, akielezea matamanio yake ya kucheza sambamba na Lionel Messi msimu ujao pale Camp Nou.**



"Ningesema kwa sasa ningeipa AC Milan faida kidogo na City faida kidogo. Kwa sababu ya uimara wao wa ulinzi na labda kwa sababu Real Madrid iko hatarini zaidi katika safu yao ya ulinzi. Lakini Real Madrid ni Real Madrid; wanaweza kufunga dhidi ya mtu yeyote, na ndiyo maana hili liko wazi," **Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, akiweka utabiri wake kwa Manchester City kukutana na AC Milan kwenye Fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu. City itakutana na Real Madrid nusu fainali huku AC Milan ikikutana na majirani zao, Inter Milan.**



"Sikiliza, sitasimama hapa na kusema naipenda, au kwamba napenda. Sipendi. Nataka kucheza kila mchezo na nimefanya kwa miaka minane iliyopita ya kazi yangu. Pia ninapaswa kuheshimu kocha na maamuzi yake na pia kuheshimu jinsi ushindani ulivyo mzuri katika beki wa kati kwenye klabu hii. Ni hivyo, na ninaamini hivyo," **Nahodha wa Manchester United, Harry Maguire, akikiri kukerwa na kukosa muda wa kucheza Old Trafford chini ya Erik ten Hag.**





UTHAMANI wa wachezaji wa soka kwenye soko la uhamisho huamuliwa na mambo mbalimbali kama vile umri wa mchezaji, urefu wa mkataba, kiwango cha wakati huo na uwezekano wa kuendelezwa siku zijazo.

Uk. 12&13



Beki wa Simba, Henock Inonga (kulia), akimdhibiti straika wa Wydad Athletic Club, Bouly Sambou kwenye mechi ya mkondo wa pili ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyopigwa Uwanja wa Mohamed wa Tano Ijumaa iliyopita. Simba ilitolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani. **MPIGAPICHA WETU**

# SABABU 5 WYDAD KUITOA SIMBA CAF

**Na Adam Fungamwango**

USIKU wa Ijumaa iliyopita, wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba walihitimisha safari yao kwenye hatua ya robo fainali, walipotolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya Mabingwa Watetezi, Wydad Athletic Club yenye maskani yake Casablanca nchini Morocco.

**Penalti zilipigwa kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano, baada ya mabingwa hao kufurukuta na kushinda bao 1-0 lililoowekwa wavuni na Msenegal Bouly Sambou, hivyo ubao kusomeka bao 1-1 kwa matokeo ya jumla, kwani Aprili 22, Simba ikiwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam ilishinda bao 1-0.**

Inakuwa ni mara ya nne kwa Simba kuishia hatua hiyo kwenye michuano ya kimataifa kwa misimu mitano ambayo imecheza, na mara tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mara ya kwanza ilikuwa ni mwaka 2019 ilipotolewa dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, baada ya suluhu nyumbani ilikwenda kupigwa mabao 4-1 mjini Lubumbashi na mwaka 2021 ilikomea hatua hiyo kwa kuondolewa dhidi ya Kaizer Chiefs ya Aftrika Kusini jumla ya mabao 4-3, ilianza kupoteza mabao 4-0 ugenini, na ikashinda nyumbani 3-0.

Mwaka jana iliishia pia hatua kama hiyo kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, ilipotolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini baada ya kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Kwenye mechi dhidi ya Wydad Casablanca, Simba ilionekana kama iko karibu zaidi kufuzu hatua ya nusu fainali, lakini kuna vitu kadhaa ambavyo vilikosekana, au kusababisha kuishia hatua hiyo.

Katika makala haya, tunakuorodheshea sababu kadhaa ambazo zilisababisha Simba kushindwa kutinga hatua ya nusu fainali dhidi ya mabingwa watetezi hao, twende sasa...

**1. Kutotumia vema uwanja wa nyumbani**

Simba inaonekana kutojipanga vema kutumia uwanja wa nyumbani kwenye hatua hizi za robo fainali. Pamoja na kwamba huwa na uwezo wa kushinda hata mabao 3-0 au hata 7-0 kama ilivyofanya dhidi ya Horoya ya Guinea, lakini inapofika hatua hiyo inashinda mabao machache ambayo yanawagharimu kwenye mechi ya marudiano.

Rejea mechi dhidi ya TP Mazembe 2019 ilipolazimishwa suluhu kwenye mechi ambayo ilipaswa kufunga mabao kadhaa, lakini pia 2022 ilipofunga bao 1-0 dhidi ya Orlando Pirates. Kama ingefunga angalau 2-0 ingeweza kufuzu hatau ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho, na kama ingeshinda mabao kadhaa dhidi ya TP Mazembe ingeweza kuipa mlima mrefu kwao.

Simba ilikuwa na uwezo wa kushinda mabao mengi kwenye mechi iliyopita dhidi ya Wydad Casablanca nyumbani kwani wachezaji wake walipoteza nafasi kadhaa, zikiwamo mbili za Clatous Chama na Pape Sakho kubaki ana kwa ana na kipa, lakini walishindwa. Iwapo ingetumia nafasi hizo, saa hizi Simba ingekuwa inajiandaa kucheza nusu fainali dhidi ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

**2. Makosa binafsi ya wachezaji**

Ukiangalia kwenye mechi nyingi hasa za kimataifa, mabao ambayo Simba inaruhusu siyo ya kimfumo, bali ni makosa binafsi ya mchezaji mmoja mmoja, hasa Joash Onyango.

Kwenye mechi za kimataifa hasa msimu huu tayari amesababisha penalti tatu, na makosa mengine ambayo yamesababisha mabao kadhaa yaliyoigharibu Simba.

Ijumaa iliyopita, bao ambalo Wydad Casablanca walifunga pia lililotokana na kosa binafsi la Onyango.

Kwanza aliutoa nje na kuwa kona mpira ambao kipa Ally Salim alikuwa ameshafika kuukamata, lakini mawasiliano yakawa hafifu.

Na kona hiyo ilizaa kona nyingine ambayo ndiyo iliyosababisha bao pekee kwenye mechi hiyo. Na hata mfungaji alipopiga kichwa, Onyango alizubaa na kuuruhusu mpira kudunda mbele yake. Hakujishughulisha hata kumbugudhi mpigaji asiwe huru.

**3. Mipira mirefu**

Kwenye mechi hiyo ukitazama, Simba ilikuwa ikipiga mipira mirefu hasa mabeki na viungo. Afadhali ile iliyopigwa pembeni ilikuwa ikidhibitiwa vizuri na kina Kibu Denis, Chama na Saido Ntibazonkiza, lakini ile ya katikati yote ilikuwa ikimezwa na mabeki wawili wa Wydad pamoja na kiungo wao mkabaji ambao wote walikuwa wanakaa na straika mmoja tu, Jean Baleke.

Beleke hakuwa na cha ziada dhidi ya mabeki hao warefu wenye nguvu ambao walikuwa wamesimama na mtu mmoja tu.

Simba walitumia mfumo sahihi ambao uliwadhibiti wapinzani wao, lakini kosa walilokuwa wakifanya ni kupiga mipira mirefu ambayo ilikuwa inachukuliwa tena na adui. Labda mbele kungekuwa na mtu kama mshambuliaji wao wa zamani, Chris Mugalu, mwenye nguvu na uwezo wa kushindana na mabeki wawili, akakaa na mpira. Kama wangejiamini na kwenda na soka la pasi walizoezoea kama ambavyo walikuwa wakifanya mara moja moja, wangekuwa hatari zaidi kwa wapinzani wao.

**4. Kiungo mkabaji bado tatizo**

Bado tatizo la namba sita asilia linaendelea kuitafuna Simba, kwani inaonekana hata makosa binafsi yanayofanyika hayasaidiwi na mwingine kutokana na kutokuwa na namba sita.

Miaka kadhaa nyuma, Thadeo Lwanga alikuwa ana uwezo wa kurekebisha au kusawazisha makosa ya wenzake kwa sababu alikuwa ni namba sita asilia.

Mzamiru Yassin Na Sadio Kanoute ukiwatazama wote wale ni namba nane, wanacheza kwa kubadilishana nafasi. Nina uhakika kama Simba ingekuwa na namba sita asilia eneo ambalo Bouly Sambou alifunga, kama namba sita angecheza Lwanga au James Kotei enzi zake asingeruhusu mpira uzagae eneo lile.

**5. Kikosi finyu**

Angalia mabingwa watetezi, kipindi cha pili watatoa wachezaji watatu na wanaingiza wengine watatu, baadaye wanatoa wawili wanaingiza mashine mbili. Ina maana ndani kuna nusu nzima ya wachezaji wapya, dhidi ya wale wale 11 wa wapinzani ambao walianza tangu mwanzo.

Simba ilianza kuingiza wachezaji kuanzia dakika ya 80 kuendelea na ilionekana ni kwa sababu ya penalti. Nao ni Erasto Nyoni na Moses Phiri.

Simba ndiyo timu pekee kwenye Ligi ya Mabingwa ambayo haipumzishi wachezaji mpaka ifikie dakika 15 au 10 kabla mechi kumalizika. Hii ina maana wanaokaa benchi wengi wao hawana viwango ama vya kucheza mechi za kimataifa, au kuchezea Klabu ya Simba.

Kuna wachezaji hao hao tegemezi kuwachosha sana, ikizingatiwa wenzao wanakuwa wameshaingiza wachezaji wengine ambao wana uwezo kama wale au kushinda. Na hii ilionekana pia kwenye mechi ya Ijumaa dhidi ya Wydad Casablanca.

**JE, WAJUA?**

AL AHLY ya Misri ndiyo klabu iliyofanikiwa kucheza nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika mara nyingi zaidi (19) katika historia ya michuano hiyo, ikifuatiwa na Esperance Sportive de Tunis ya Tunisia (14), TP Mazembe ya DR Congo (12), Zamalek ya Misri (10), Asante Kotoko Sporting ya Ghana (10) na Wydad Athletic Club ya Morocco (9).





# MOI yaandika historia matibabu kichwa, mgongo

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI) imezindua huduma mpya ya kibingwa ya matibabu ya maumivu sugu ya mgongo na kichwa bila upasuaji.

Matibabu hayo tangu yazinduliwe hivi karibuni yameshawanufaisha wagonjwa 20 ambao walitibiwa hospitalini huko na wanaendelea vizuri.

Huduma hiyo ambayo ni mpya nchini, imeanzishwa kwa ushirikiano kati ya MOI na Hospitali ya YASHODA ya India.

Akizungumza katika ofisi za taasisi hiyo juzi wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface, alisema wameanzisha huduma hiyo ili kutekeleza agizo la serikali la kuhakikisha Tanzania inakuwa kituo cha utalii wa matibabu. "Kama mnavyofahamu, Mheshimiwa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan, ana msukumo mkubwa wa kuifanya nchi yetu kuwa kitovu cha utalii wa matibabu katika Ukanda wa Afrika Mashariki, Kati na Kusini, hivyo kuanza kwa huduma hii ni sehemu ya mkakati wetu wa kutekeleza kwa vitendo maono hayo ya Mheshimiwa Rais," alisema Dk. Boniface Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Utalii wa Matibabu, Abdulmalik Mollel, alisema ni muda mwafaka kwa Tanzania kuwa kituo cha utalii wa matibabu kutokana na uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali kwenye sekta ya afya.

Alisema kupitia uwekezaji huo mkubwa, hivi sasa huduma nyingi za kibingwa na kibobezi zinapatikana kwenye hospitali mbalimbali za nchini.

Alisema uwekezaji huo umefanywa kwenye ununuzi wa vifaa vya teknolojia ya kisasa ya matibabu ya aina mbalimbali ambayo hata nchi jirani zimekuwa zikija kujifunza.

Alisema kwa uwekezaji uliofanywa na serikali, Tanzania imeanza kupokea wagonjwa wengi kutoka nje na wale waliokuwa wakienda nchi zilizoendelea kama Marekani, India na za barani Ulaya kwa matibabu, sasa wanaweza kuja nchini na kupata huduma zinazopatokana kwenye mataifa hayo. Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya YASHODA, India, Dk. Ravi Suman Reddy, alisema ushirikiano kati yao na MOI utaleta manufaa makubwa kwa watanzania na mataifa mengine ya Afrika Mashariki na Kati ambako huduma hizo hazipatikani.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mgongo na Ubongo MOI, Dk. Nicephorus Rutabasibwa, alisema kambi hiyo itakuwa na matokeo chanya kwa huduma za kibingwa nchini kwa kuwa huduma hizo zitaendelea kutolewa MOI hata baada ya wataalamu kutoka India kuondoka na hivyo kuwaondolea usumbufu wagonjwa kufuata huduma nje ya nchi.




Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Mayamaya wilaya ya Bahi Jonathan Chibalangu (kushoto) akipokea mfuko wa simenti kati mifuko 153 iliyotolewa na Meneja wa Biashara kanda ya kati taasisi ya Sanlam Dodoma, Said Makongwa (kulia) kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mayamaya.**PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jela miaka 30 kwa kubaka

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi mkoa Geita imemhukumu Elisha James (47), mkazi wa Kijiji cha Kishimbazobe, kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la kubaka mwanamke mwenye umri wa miaka 25 na kumsababishia maumivu sehemu za siri.

Hukumu hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Johari Kijuwile mwishoni mwa wiki baada ya mshtakiwa huyo kukiri kosa la kumbaka mwanamke huyo.

Baada ya James kukiri kosa, Hakimu Kijuwile alimtaka Wakili wa Serikali Venance Mkonongo amsomee mshtakiwa maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Venance Mkonongo alidai mahakamani huko kuwa mshtakiwa alimbaka mwanamke huyo (jina tunalo) ambaye siku ya tukio, Machi 13 mwaka huu, alikuwa amelala na mtoto wake na mama yake mzazi katika Kijiji cha Kishimbazobe, Wilaya ya Geita.

Alidai kuwa mama mzazi wa mwanamke huyo aliondoka kwenda shambani majira ya saa 12 asubuhi na kumwacha bintiye amelala na mtoto wake, lakini hakufunga mlango, ndipo mshtakiwa alipoingia ndani ya chumba alichokuwa amelala mwanamke huyo pamoja na mtoto wake na kuanza kumkaba huku akiwa amemziba mdomo na alipotimiza haja zake, alikimbilia kusikojulikana.

Alidai kuwa mwanamke huyo alikwenda kwa mjumbe kutoa taarifa na mjumbe akamtaka kutoa taarifa Kituo cha Polisi Geita ambako alipewa alipewa kibali (PF3) na kwenda Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Geita kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Wakili huyo alidai uchunguzi wa daktari ulionyesha mwanamke huyo alibakwa. Baada ya polisi kupata taarifa za uchunguzi wa daktari, walimsaka mtuhumiwa huyo na kumkamata na baada ya mahojiano mtuhumiwa huyo alifikishwa mahakamani na aliposomewa shtaka lake alikiri kumbaka mwanamke huyo.

Baada ya Wakili wa Serikali Mkonongo kumaliza kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali, Hakimu Kijuwile alisema "kwa kuwa mshtakiwa umekiri kosa lako mwenyewe bila kulazimishwa, mahakama hii inakutia hatiani kwa kosa ulilosthakiwa nalo. Pia inakutaka ujitetee ili kukupunguzia adhabu."

Mshtakiwa huyo alijitetea "ni kweli mimi nimebaka, ninaomba mahakama hii inipunguzie adhabu, hili ni kosa langu la kwanza".

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkonongo ulidai mahakamani kuwa makosa ya unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji mkoani Geita yamekuwa mengi, hivyo ukaiomba mahakama itoe adhabu kali kwa mshtakiwa huyo ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine wenye tabia za kubaka.

Hakimu Kijuwile alitupilia mbali utetezi wa mshtakiwa na kusema kitendo alichokifanya ni cha kikatili - kuingia kwenye chumba cha mtu na kumbaka. Alikitaja ni kitendo kisichokubalika katika jamii, hivyo akamhukumu kifungo cha miaka 30 jela.


IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM

CIVIL APPEAL NO. 05 OF 2021

TANZINDIA ASSURANCE COMPANY LIMITED..............................................APPELANT

VERSUS

MGEN TANZANIA INSURANCE COMPANY LIMITED.......................................1ST RESPONDENT

PIUS CHARLES MABUBULWA........2ND RESPONDENT

GUMADA INVESTMENT LIMITED......3RD RESPONDENT

TO:
PIUS CHARLES MABUBULWA.
DAR ES SALAAM
SUMMONS FOR PUBLICATION

Whereas the plaintiff has instituted a suit against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by a pleader duly instructed and able to answer all material question relating to the suit or who shall be accompanied by some person able to answer all such question on the 23RD day of May,2023 at 08:00am, o'clock before Hon. E. Kisanya , J to answer the suit, you must be prepared to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

Take notice that, in default of your appearance on the day before mentioned the suit will be heard and determined in your absence given under my hand and the seal of this court on 4th day of April 2023

DEPUTY REGISTRAR

IN THE HIGH COURT OF TANZANIA
(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)
AT DAR ES SALAAM

CIVIL APPEAL NO. 05 OF 2021

TANZINDIA ASSURANCE COMPANY LIMITED..............................................APPELANT

VERSUS

MGEN TANZANIA INSURANCE COMPANY LIMITED.......................................1ST RESPONDENT

PIUS CHARLES MABUBULWA.........2ND RESPONDENT

GUMADA INVESTMENT LIMITED......3RD RESPONDENT

TO:
GUMADA INVESTMENT LIMITED.
DAR ES SALAAM

SUMMONS FOR PUBLICATION

Whereas the plaintiff has instituted a suit against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by a pleader duly instructed and able to answer all material question relating to the suit or who shall be accompanied by some person able to answer all such question on the 23RD day of May,2023 at 08:00am, o'clock before Hon. E. Kisanya , J to answer the suit, you must be prepared to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your defence.

Take notice that, in default of your appearance on the day before mentioned the suit will be heard and determined in your absence given under my hand and the seal of this court on 4th day of April 2023

DEPUTY REGISTRAR

KUPOTEA KWA CHETI



**JULIA BARAKA KIBOGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S.0313.0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **IKIZU SEKONDARI** mwaka **2003.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/93124/2021.**

FORM NO. 58
IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE
OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO. 23 OF 2023

In Matter of the Estate of the Late
RUWAICHI PAULO MAMBALI

By 1. ASANIEL GILBERT MAMBALI
2. ..................................

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the DISTRICT COURT **3rd /May / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this.....day of... **2023**

KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA DODOMA

UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI

SHAURI LA MIRATHI NA. 4 YA 2023

Maombi ya barua za usimamizi wa Mirathi ya
ELIAKIM PAUL MARTIN MREMA..................MAREHEMU

NA

JACOB ELIAKIM MREMA............................ MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75 na 76)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya Marehemu alietajwa hapo juu, wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji alietajwa hapo juu.
Mapinagamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 09 mwezi Mei mwaka 2023.
Imetolewa leo Tarehe 21 Mwezi wa Aprili, 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
DODOMA

117405201





# Viongozi wa dini wapiga marufuku taasisi kutetea mapenzi jinsia moja

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa dini mkoani Mbeya, wamepiga marufuku taasisi yoyote kutetea mapenzi ya jinsia moja kwa kutumia mwamvuli wa dini na kwamba vitendo hivyo ni vya 'kishetani' na sio sehemu ya haki za binadamu kama inavyodaiwa.

Marufuku hiyo waliitoa mwishoni mwa wiki jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Amani ya viongozi wa dini na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (NEC) Taifa, anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela.

Kamati hiyo inawahusisha viongozi wa dini ya Kiislamu na Kikristo ambayo imeundwa kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika kushughulikia mambo mbalimbali ya kijamii ikiwamo kukemea mambo maovu.

Katibu wa Kamati hiyo, Askofu Geofrey Mwakihaba, alisema kuna baadhi ya makundi yanayodai haki hizo za mapenzi ya jinsia moja, yanatumia biblia kudai haki hizo na kutumia baadhi ya vifungu ambavyo havimo kwenye vitabu hivyo vitakatifu na kupotosha umma.

Mwakihaba ambaye ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, alisema makundi hayo yanaweza yakatumia dini kwa kisingizio cha serikali haina dini.

"Tuna taarifa kwamba baadhi ya makundi yanatumia mwamvuli wa dini kuhalalisha uchafu huu, bahati nzuri wenzetu waislamu mna nafuu sijasikia kama Quran inatumika kwenye uchafu huu, sasa msimamo wetu ni kwamba hakuna dini inayoruhusu mambo haya hivyo lisijitokeze kundi lolote kuendelea kutumia dini," alisema Mwakihaba.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Shekhe Ayas Njalabaha, alisema vitendo hivyo vimeanza kukithiri nchini na kwamba ni wajibu wa viongozi wa dini kukemea ili vikome kujenga taifa lenye maadili. Njalabaha, ambaye ndiye Shekhe wa Mkoa wa Mbeya, alisema vitendo hivyo vimekuwa vikifanyika kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo shule za bweni na baadhi ya maeneo ambayo yanaaminika.

Aliiomba serikali kutumia vyombo vyake vya ulinzi na usalama kudhibiti vitendo hivyo na kuongeza ukali wa sheria kwa wanaojihusisha na vitendo hivyo ili watu wawe wanaogopa kufanya.

"Kwa sasa tunakabiliwa na tatizo hili la mmomonyoko wa maadili kwenye maeneo mbalimbali, sasa ni wajibu wetu sisi viongozi wa dini kushirikiana na serikali kukemea na kuelimisha jamii kuhusu ustaarabu wetu," alisema Shekhe Njalabaha.

Mwakilishi wa Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mbeya, Padri Telesphory Tweve, alisema mapenzi ya jinsia moja sio haki za binadamu na viendo hivyo vilimchukiza Mungu wakati wa Sodoma na Gomola na aliamua kukiteketeza kizazi cha wakati huo. Alisema kutokana na hali hiyo, wanaodai haki hiyo hawatakiwi kuwadai wanadamu wenzao na badala yake wamdai Mungu ambaye ndiye aliyeumba ustaarabu uliopo kwa sasa.

Aliiomba serikali kuzishughulikia taasisi mbalimbali ambazo hivi karibuni zilitajwa kuwa zinahusika na kampeni hizo haramu pamoja na kuzuia misaada kutoka nje ambayo inabainika kuwa na viashiria vya kushawishi 'ushetani' huo.

Mjumbe wa NEC anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Mwaselela aliwapongeza viongozi hao kwa kuungana na serikali kupiga vita vitendo hivyo akidai kuwa serikali pia inafanya jitihada mbalimbali kuvikomesha.

Alisema hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, alionyesha msimamo wake kwamba vitendo hivyo havikubaliki nchini na nguvu ya viongozi wa dini inaongeza mapambano hayo.



Mganga Mkuu wa mkoa wa Songwe Dk. Boniface Kasululu akizungumza jambo na wadau katika uzinduzi wa chanjo zote hafla iliyofanyika mwishoni mwa wiki mkoani humo. **PICHA: YASINI IBRAHIM**

# RC aagiza upanuzi hospitali ya wilaya kukamilika Mei 25

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imetakiwa kusimamia mradi wa upanuzi wa hospitali ya wilaya hiyo na kuhakikisha unakamilika kabla ya Mei 25 mwaka huu ili wananchi waendelee kupata huduma.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipoweka jiwe la msingi la upanuzi wa hospitali hiyo huku Serikali Kuu ikitoa zaidi ya Shilingi bilioni moja kwa ajili ya upanuzi na ununuzi wa baadhi ya vifaa.

Alisema majengo yanayojengwa kwenye hospitali hiyo likiwamo jengo la wajawazito kusubiri kujifungua yanatakiwa kujengwa kwa viwango vinavyokusudiwa na serikali ili thamani halisi ya fedha ionekane.

Alisema baada ya muda huo kuisha atakwenda katika wilaya hiyo kwa ajili ya kuyazindua majengo hayo ili yaendelee kufanya kazi ya kuwahudumia wananchi.

Pia, alisema serikali iliamua kuipanua hospitali hiyo ili kusogeza huduma mbalimbali kwa wananchi wa wilaya hiyo na kupunguza msongamano kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya na Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya.

"Hapa kuna jengo ambalo linajengwa na wenzetu UNICEF (Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto), waambieni wajaribu kuongeza kasi ili nalo likamilike haraka na lianze kutoa huduma kwa wananchi," alisema Homera.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaimarisha huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga zahanati katika kila kijiji, Kituo cha Afya katika kila Kata na Hospitali ya Wilaya kwenye kila wilaya ili wananchi wasitumie muda mrefu kutafuta huduma hiyo.

Alisema hospitali ya wilaya inatakiwa itumike kama rufani kwa wagonjwa ambao wanashindwa kuhudumiwa kwenye zahanati na vituo vya afya. Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, aliahidi kusimamia kwa weledi utekelezaji wa mradi huo ili ukamilike kwa wakati kama walivyoelekezwa na watahakikisha ubora wa mradi huo unatekelezwa kama serikali ilivyokusudia.

Alisema baadhi ya majengo yameshakamilika na yanatumika kutoa huduma na baadhi yako katika hatua za mwisho kukamilika na kuahidi kuwa mpaka kufikia tarehe waliyopewa na Mkuu wa mkoa watakuwa wamekamilisha. Aliyataja baadhi ya majengo yaliyokamilika kuwa ni pamoja na la mionzi ambalo tayari baadhi ya vifaa vimeshawekwa na kuanza kutoa huduma ikiwamo mashine ya X-Ray ya kisasa.

"Majengo mengine kama ulivyoona yako katika hatua za mwisho kabisa, naahidi kwamba tutayakamilisha ndani ya muda ulioutaja hapa na yataanza kutoa huduma," alisema Mayeka.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chunya, Ramadhan Shumbi, alisema watasimamia ujenzi wa majengo hayo na kuhakikisha yanakuwa na ubora unaotakiwa.

# Madiwani wapewa kazi kusimamia usafi wa jiji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wametakiwa kusimamia usafi katika maeneo yao kwa kuhakikisha taka zinazokusanywa na wananchi zinatolewa kwa wakati ili kulifanya jiji kuwa safi na kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, alitoa agizo hilo kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo cha robo ya mwisho wa mwaka wa fedha 20222/2023 ambayo alisema kuna baadhi ya maeneo bado ni machafu.

Alisema madiwani wakishindwa kusimamia usafi kwenye maeneo yao hatua zitaanza kuchukuliwa kutokana na baadhi ya matatizo kusababishwa na wao wenyewe.

Alisema uzoaji wa taka kwa kuwatumia wazabuni ulionekana kuwa ndio mwarobaini wa kumaliza tatizo la uchafu katika jiji hilo, lakini kwa sasa imeanza kuonekana kuna matatizo pia.

"Wananchi wanakusanya takataka barabarani, lakini zinapita siku kadhaa gari la kuzoa taka hizo haliji, ninyi madiwani ambao ndio wenyeviti wa kamati za maendeleo kwenye kata zenu mnatakiwa kusimamia vizuri jambo hili," alisema Malisa.

Alisema wananchi wanachangia gharama za kuzoa taka hizo kila mwezi, lakini ufanisi wa uzoaji wa taka hizo ni mdogo jambo ambalo linawakatisha tamaa wananchi hao.

Ofisa Mazingira wa Jiji la Mbeya, Nimrood Kiporoza, alikiri kuwapo kwa tatizo la baadhi ya wazabuni kuziondoa taka zinazokusanywa na wananchi na tayari wameshaanza kuweka mikakati ya kukabiliana na tatizo hilo.

Alisema watawachukulia hatua za kisheria wazabuni hao kulingana na makubaliano yaliyomo kwenye mikataba yao.

Meya wa jiji hilo, Shekhe DorMohamed Issa, alisema ili kuhakikisha ufanisi unaongezeka wameanzisha utaratibu wa taka hizo kuondoshwa usiku magari yanayosafirisha kwenda kwenye ghuba kuu lililopo Nsalaga yasikwame.



# Uongozi Seeds of Light waishukuru serikali kuondoa taharuki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UONGOZI wa Shule ya Seeds of Light ambayo ilituhumiwa kufundisha mapenzi ya jinsia moja kwa wanafunzi wa shule hiyo, umesema kuwa hatua ya Serikali ya Zanzibar kupitia Wizara ya Elimu kufanya uchunguzi na kujiridhisha haihusiki na tuhuma hizo imesaidia kuondoa taharuki kwa wazazi wa wanafunzi na wanakijiji wa kijiji hicho.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mkurugenzi wa shule hiyo, Cosiano Ismail Mbise, alisema kutoka kwa taarifa hizo za shutuma katika mitandao ya kijamii ilizusha taharuki kubwa kwa wazazi, wanakijiji hicho na taifa kwa ujumla hali ambayo ilifikia wazazi kukosa imani na uongozi wa shule hiyo.

Alisema wazazi walitaka kuchukua uamuzi ya kuwatoa shule watoto wao, lakini baada ya taarifa ya serikali ya kujiridhisha na ufundishaji wa shule hiyo imesaidia kubadili mawazo yao. Mkurugenzi huyo alizitaka taaisi zinazohusika na mitandao ya kijamii, kufuatilia matumizi sahihi ya mitandao hiyo kwa sababu baadhi inazusha taharuki na baadhi ya taarifa huwa sio sahihi.

Aidha, alisema uongozi wa shule ulifuatilia mtandao uliorusha taarifa hizo za uzushi, lakini alivunjika moyo baada ya kwenda katika vyombo vinavyosimamia mitandoa hiyo kuelezwa kuwa mrushaji wa taarifa hiyo ni mtu aliyefahamika hivyo hawezi kutambulika.

Alikiri kuwa shuleni hapo ilikuwapo picha ya nembo ya upinde (Rainbow), lakini uwapo wa mchoro huo haukuwa na maana ya kuunga mkono mapenzi ya jinsia moja na wala hawakudhania kuwa hali hiyo itawaudhi watu.

Mbise alisema wameshafuata mwongozo wa Wizara ya Elimu Zanzibar ya kufuta nembo hizo na kuwataka wazazi na jamii yote kuendelea kutoa ushirikiano katika kusogeza mbele gurudumu la elimu.

Alisema kuwa lengo la shule hiyo ni kutoa elimu kwa wananchi wa kiwango cha chini na taasisi inayoendesha shule hiyo ndiyo inayogharamia gharama zote za wanafunzi katika kupata elimu bora ili kuwasaidia wananchi wa kijiji hicho kuwa na vijana wasomi baadaye na kukuza kiwango cha elimu kwa wanafunzi.

Naye Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Innocent Frank Maile, alisema shule hiyo imelenga kuwatengenezea maisha bora watoto yenye mwanga mzuri unaozingatia maadili.

Alisema awali walipoanza kupokea wanafunzi mwaka 2020 kiwango cha elimu kwa watoto wa kijiji hicho kilikuwa chini kutokana na wazazi na jamii husika kuwa na mwitikio mdogo katika kuwasaidia watoto wao katika elimu.

"Ilifikia hatua Mtoto unampa homework ili aende akafanye nyumbani, siku ya pili anarejea shule hakuna kazi iliyofanyika na daftari lipo tupu kwa sababu wazazi hawakua na mwamko wa umuhimu wa elimu, lakini sasa tunashukuru hali imebadilika na wazazi wanashiriki vizuri katika kujua maendeleo ya elimu ya watoto wao," alisema.

Alisema tayari wameshayafanyia kazi upungufu wote ulionekana shuleni hapo.

Hivi karibuni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kupitia waziri Lela Mohammed Mussa, ilisema baada ya kupata taarifa ya uwapo wa tuhuma ya shule inayomilikiwa na taasisi ya CR Hop Foundation chini ya mmiliki wake Renos Fountoulatis ambae ni raia wa Ugiriki imejirisha na kufanya uchunguzi baada ya kufanya uchunguzi na kubaini kuwa haihusiani na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na maadili.

## Uchafu wa mazingira maeneo ya fukwe watisha

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

HALI ya kimazingira katika fukwe za bahari bado ni changamoto kutokana na mvua za masika zinazoendelea kunyesha.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa uhifadhi wa bahari Zanzibar, Dk. Makame Omar Makame, katika hafla ya usafishaji wa fukwe eneo la Fumba.

Alisema hali ya mazingira haiko vizuri katika fukwe kutokana na mvua za masika na kusababisha nyingi kuharibika kwa taka hasa chupa za plastiki kutokana na maji ya mvua kumwaga maji yake katika bahari.

Alisema katika kuhakikisha kuwa hali ya kimazingira inakuwa vizuri ndiyo maana wafanyakazi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, wakaamuwa kutenga muda wao na kusafisha mazingira katika diko hilo na maeneo mingine ya Unguja na Pemba.

Naye Mkurugenzi uendeshaji utumishi kutoka wizara hiyo, Issa Suleiman Ali, alisema wametenga muda huo kufanya usafi kama njia moja ya kuilinda bahari na uharibifu wa mazingira.

Alisema wafanya kazi wa wizara huyo wana wajibu wa kuhakikisha kuwa bahari ipo salama wakati wote ili kufikia malengo ya kuwapo kwa uchumi wa buluu na mipango yake ya kuwanufaisha wananchi.

Aidha, jitihada zilizofanywa na wizara hiyo katika kuifanya bahari kuwa ni moja ya ajira wananchi wengi hivi sasa wamehamasika ukulima wa mwani, ufugaji wa samaki na matango bahari.




Mwalimu Mkuu wa Shule ya Seeds of light iliyopo Kizimkazi mkoa wa kusini Unguja, Innocent Frank akionesha kitabu wanavyofundishia shuleni hapo, baada ya kumalizika kwa kikao baina ya uongozi wa shule na waandishi wa habari, kufuatia taarifa ya wizara ya elimu kujiridhisha na uwepo wa shule hiyo baada ya kusambaa kwa taarifa za uzushi kuwa shule hiyo inajihusisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja na kufundisha wanafunzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN.**

# Wadau kukutana leo Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa habari na waandishi wa habari 300 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar wanakutana leo visiwani humo kwa ajili ya kuadhimisha siku ya uhuru wa vyombo vya habari ambayo itaammbatana na kongamano na mada mbalimbali zitawasilishwa. Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa kamati ya maandalizi ya uhuru wa vyombo vya habari ambayo yanafikisha miaka 30, Dk. Rose Ruben, alisema mada tatu zitawasilishwa katika kongamano hilo na Mei 3, katika kilele cha maadhimisho hayo yatakayofunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Dk. Rose alisema kupitia taasisi mbalimbali za habari wanaridhishwa na kazi kubwa inayofanywa na viongozi wakuu wa nchi mbili katika kuleta mageuzi ya taaluma hiyo ili ifanye kazi zake vizuri na kutoa taarifa kwa umma.

Alisema kutakuwa na mada mbalimbali ikiwamo usawa wa kijinsia, mazingira na usalama wa ufanyaji kazi kwa waandishi wa habari na kujadili, kuzungumzia Sheria za Habari ambazo zinagusa utendaji wa kazi. "Ujumbe wa mwaka huu katika maadhimisho haya ni 'Kuunda mustakabali wa haki na uhuru wa kujieleza kama kichocheo chengine cha haki ya binaadamu'," alisema.

Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, alisema katika maadhimisho hiyo lengo ni kujenga tasnia ya habari ili kuwa jambo la Watanzania kujivunia.

Alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, zimeazimia kuifanya taaluma ya habari kuwa bora zaidi ikiwamo kukubali kufanyika kwa marekebisho ya sheria ziliopo ili kwenda na wakati wa mabadiliko.

Alisema Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele kuona taaluma ya habari inaleta mabadiliko makubwa ya maendeleo ikiwamo kuwapo kwa uhuru wa habari unaokwenda na mabadiliko ya wakati wa sayansi na teknolojia.

Alisema hatua hiyo ilimfanya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kukubali mchakato mzima wa kuwapo kwa marekebisho ya Sheria ya Habari ambayo ni rafiki kwa waandishi wa habari katika utekelezaji wa majukumu yake ya kazi.

Alisema katika kuona waandishi wa habari wanapata sheria yenye kukidhi mahitaji yao, tayari Waziri wa Habari, Teknolojia ya Habari wa Serikali ya Muungano, Nape Nnauye amewasilisha marekebisho ya sheria hiyo katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Habari (MAELEZO) Zanzibar, Hassan Khatib, alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeonesha njia ya kufanya kazi na waandishi wa habari katika kuleta mageuzi ya maendeleo na kuona taarifa zinawafikia walengwa.

Alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi alipoingia madarakani ameanzisha utaratibu wa kuzungumza na waandishi wa habari kila mwezi hatua inayoisaidia jamii kwa kiasi kikubwa kujua matukio mbalimbali yanayofanyika nchini.

URAFIKI WA SIASA VS WAFANYAKAZI UNAVYODUMU

# Samia aendeleza ubunifu wa Nyerere na Kawawa, zama harakati uhuru 1955

**Na Peter Orwa**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

LEO wafanyakazi wako katika Sikukuu yao. Inapoangaliwa kwa kina, ni mnyororo mrefu, mzizi wa Mapinduzi ya Viwanda Ulaya, ikiwamo kwa waliotawala nchini, Taifa la Uingereza.

Kuibuka kada kubwa ya wafanyakazi, walioanza kukumbwa na dai la kuonewa, pia kunyanyasika, ikaibua dai la uhuru na haki kazini. Zao lake ikawa kuzaliwa vyama vya wafanyaazi, hali kadhalika sheria zinazowalinda, ikienda mbali na kuunda urafiki na wanasiasa.

Kwa taifa Uingereza, kukaibuka jamii ya watu ambao walikuwa ahueni na wana utashi wa kisiasa waitwao 'Fabian Society, wakawa bega kwa bega na wafanyakazi. Nyendo zao zilifika hatua ya kuunda chama cha kisiasa kilichoitwa 'Labour'mwaka 1900, ambayo tafsiri yake ni 'kazi'. Hapo ukaundwa uswahiba mkubwa kati ya nyendo za wafanyakazi na wanasiasa.

Hadi leo hii karne kadhaa zimepita, chama hicho ni kikubwa sana, kikiwa mshindani mkuu chama cha Conservative, ambacho kina mzizi wa vigogo wamiliki uchumi ikiwamo viwanda Uingereza.

### KINACHOJIRI NCHINI

Tanzania nako kuna mzizi kama huo wa urafiki wa siasa na harakati za wafanyakazi. Ilikuwa wakati huo Mwenyekiti wa TANU, Mwalimu Julius Nyerere, akiwa na chama kichanga kwenye harakati zake kusaka uhuru, alivutiwa sana na kazi iliyokuwa kwenye chama cha wafanyakazi (TFL- Tanganyika Federation of Labour ) wakati huo na kwa namna ya upekee, Katibu Mkuu wake kijana, Rashid Mfaume Kawawa.

Ilikuwa mwaka 1955 katika namna ya pekee, Kawawa akaongoza migomo ya wafanyakazi nchini, hata ikiwekwa rekodi mgomo wa Wafanyakazi wa Reli (sasa TRC), chini ya kiongozi (Balozi ) Christopher Kasanga Tumbo, vilevile kama huo katika Kiwanda cha bia Dar es Salaam, hata kuitikisa serikali ya Wakoloni Waingereza kuridhia madai yao.

Kwa mujibu wa Kawawa, katika mazungumzo na mwandishi wa makala hii miongo miwili iliyopita, mwanasiasa Nyerere akaomba faragha na mfanyakazi Kawawa, katika kikao kilichofanyika ofisi ya TANU Mtaa wa Lumumba, Dar es Salaam, akitaka urafiki kati ya TFL na TANU kushikikiza serikali ya kikoloni kuelekea Uhuru wa nchi.

Kawawa anasimulia mazungumzo hayo hayakuwa magumu kwake, maana wakati Nyerere akijenga hoja kumshawishi, yeye alishavutiwa naye siku nyingi tangu yu Mwalimu hajaingia kwenye siasa, siku alipofika shuleni kwao Tabora, Kawawa akiwa mwanafunzi., Walishiriki mijada ya wanafunzi 'akimkosha' Kawawa katika stadi za lugha na kujenga hoja, akiwa wa mwalimu mwenzake (Balozi ) Tibandebage.

> Naye katika hotuba akawajibu ana taarifa 'kimeshaeleweka' jambo inayodaiwa ilikuwa na ukweli wamepata siku, umma kuangua kicheko. Nayo inaendeleza matukio yanayoweka urafiki wa siasa na wafanyakazi jirani.

Tangu mwaka 1955, TFL ikawa sehemu ya timu ya TANU kusaka uhuru na baada ya miaka kadhaa, Nyerere akamshawishi Kawawa kujiunga katika uongozi wa siasa, akitoka kwenye harakati za wafanyakazi, alikodumu muda wote.

### WAFANYAKAZI NA UHURU

Hata baada ya kupatikana uhuru wa Tanganyika, daima urafiki wa siasa na wafanyakazi haukuachana kamwe, nchi ikitangazwa ni ya wakulima na wafanyakazi, bendera ikibeba jembe na nyundo.

Ilipofika mwaka 1964 uliopatikana Muungano wa nchi, pia mfumo wa chama kimoja, wafanyakazi waliunda Jumuiya kuu za chama cha TANU na hata ilipoerejewa mfumo wa siasa huria miaka 28 baadaye 1992, vikaachwa kuwa vyombo huru.

Ni zama mifumo ya uzalishaji viwandani na huduma za kitaasisi zilimea kila namna, hata msamiati 'shida ya ajira' ulikuwa katika kiwango cha chini. Baadaye mwaka 1969, iluuda sheria ya COPo iliyosimamia maslahi ya wafanyakao wa umma.

Ilipoingia Awamu ya Pili ya Uongozi chini ya Rais Ali Hassan Mwinyi, akashuhudiwa kuendeleza yake, akiwa na miongozo, pia sera zinazopigania haki na nafasi ya mfanyakazi.

Wakati ushindani uliporomosha mifumo ya uzalishaji nchini, Rais Mwinyi akabuni Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC), ambayo ndani yake ilishika utetezi wa uzalishaji na ajira ya Watanzania, kwa kubinafsisha taasisi hizo.



Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Kuna maeneo Rais Mwinyi alichukua hatua binafsi katika maslahi ya kada muhimu kwa umma, mathalan wataaluma wa Chuo Kikuu cha Dar es Salama, wakati huo kikiwa pekee, hata ikamea kwenda kwenye vyuo vingine vya kawaida.

Ikaja zama Awamu ya Tatu, Rais Benjamin Mkapa, katika hilo akaendeleza kwa kada mathalan ya watumshi wa ulinzi na usalama, hata asakari wa Jeshi la Ulinzi kukopeshwa magari (KIA na Mitsubishi), huku mwaka 2004, akazindua kinachopigiwa makofi hadi leo, Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini.

Awamu ya Nne, ikapigia msumari katika urafiki na kundi la wafanyakazi na siasa, tabasamu kati yao ikiweka kumbukumbu ya namna yake kuzua kicheko cha umma, pale katika madhimisho mojawapo ya Mei Mosi, washiriki kada ya walimu wakiwa na kibao uwanjani cha masihara 'shemeji hapaeleweki' kwa maana ya hawajapata mshahara, akiwa mke mwalimu.

Naye katika hotuba akawajibu ana taarifa 'kimeshaeleweka' jambo inayodaiwa ilikuwa na ukweli wamepata siku, umma kuangua kicheko. Nayo inaendeleza matukio yanayoweka urafiki wa siasa na wafanyakazi jirani.

Serikali Awamu ya Tano, Rais Dk. John Magufulil katika wastani wa miaka yake sita, kuna makuuu yenye sura mbili, moja akaanza na uhakiki wa watumishi umma, huku kwenye bajeti ya mwisho ya mwaka 2021/22 akaanza kuongeza mshahara, kabla ya kufariki.

Hata hivyo, Dk. Magufuli amwaachia wafanyaklazxio fursa nyingio za ajira, kupitia viwanda vingi vipya alivyosajili, mfano hai katika viwanda vya Mkuranga mkoani Pwani na maboresho ya bandari za Tanga na Mtwara.

### AWAMU ILIYOKO

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akiwa na miaka miwili na miezi kadhaa kazini, ameonyesha kuwaunga mkono wafanyakazi, akiwaelekezea kile anachofanya kwa umma wote katika staili ya 'kurekebisha.' Ni hivi karibuni, alirejesha maslahi na stahiki zote katika kundi lile ambalo liliachishwa kutokana na mikasa ya vyeti bandia, kwa kupewa michango yao yote katika mifuko ya hifadhi ya jamii.

Ni katika urafiki huo wa siasa na wafanyakazi, akaelekeza walioachishwa kazi kimkasa wakiwa na elimu ya darasa la saba, warejeshwe kazini, huku wafanyakazio wadaiwa wa mikopo ya vyuo vikuu, akawaondolea riba zote zilizokuwa zinalalamikiwa.

Kama kawaida yake kafungua milango ya kijinsia, mifumo mingi ya utendaji kiuongozi kitaifa kuanzia baraza la mawaziri, hadi ngazi za kitaasisi, kuna idadi kubwa ya kinamama katika awamu yake ya uongozi.

Rais Dk. Samia akizungumza mwaka jana katika siku kama ya leo Mei Mosi, akaahidi kuboresha maslahi ya watumishi nchini, lengo ni kuwawezesha wamudu gharama kimaisha, akifafanua alishaagiza kufanyika majadiliano ya kuimarisha maslahi ya wafanyakazi kati ya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) na serikali, kujua kiwango cha maslahi itakayohitajika.

Kwa masihara ya kirafiki hata yakaangua kicheko, kama ya Rais Kikwete, naye Samia akatamka:"Tuliyoyafanya mwaka huu, mambo mbalimbali, kupunguza kodi...tutaendelea kuyafanya. Lakini pamoja na hayo, lile 'jambo letu lipo' (maslahi). Ndugu zangu,' jambo letu' lipo si kwa kiwango kilichosemwa na TUCTA, kwa sababu mnajua hali ya uchumi wetu...."

HABARI KIMATAIFA

## CORECU yapata mbinu kufikisha haraka pembejeo kwa wakulima

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA Kikuu Cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU) kimekubaliana kuanzisha wakala wa pembejeo za kilimo ili kuwarahisishia wakulima upatikanaji wa mbegu za mazao mbalimbali.

Wanachama wa chama hicho walifikia makubaliano hayo wakati wa mkutano mkuu uliofanyika juzi mjini Kibaha.

Akiwasilisha pendekezo hilo kwa wanachama, Meneja wa CORECU, Mantawela Hamis alisema chama hicho kinaanzisha uwakala wa pembejeo kupitia Taasisi ya Wakala wa Pembejeo za Kilimo (ASA), TARI Naliendele na nyingine zinazojihusisha na shughuli hizo.

Mantawela alisema wanatarajia kufanya hivyo kutokana na kuwapo mahitaji ya mbegu za mahindi, mpunga, alizeti, mbaazi na kunde; mazao yanastawi katika Mkoa wa Pwani.

Meneja huyo alisema kuwa kwa kushirikiana na bodi ya korosho na watalamu wa halmashauri, wakulima wamefanikiwa kusimamia na kuongeza ubora kwenye zao la korosho kutoka asilimia 72 kwa korosho daraja la kwanza msimu wa 2021/22 hadi kufikia asilimia 96.3 msimu wa 2022/23.

Kwa mujibu wa Mantawela chama hicho kimefanikiwa kuratibu upatikanaji wavipimo unyevu 20 kwa ajili ya kudhibiti ubora wa korosho. Vipimo vitagawiwa kwa vyama vya ushirika vya msingi vyenye uzalishaji mkubwa.

Mwenyekiti wa CORECU, Musa Mng'eresa aliviagiza vyama wanachama kuhakikisha vinalipa viingilio na hisa ili chama hicho kiendeshwe kwa mujibu wa sheria.

Katika mkutano huo wanachama pia walikubaliana kuanzisha kilimo cha michikichi ili kuongeza mazao ya biashara yatakayokuwa yanasimamiwa na CORECU.

# Kampuni yapongezwa kuthamini mchango wa wafanyakazi wake

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ni maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani. Serikali imeipongeza Kampuni ya Simba Bingwa kwa uanzishwaji wa tuzo kwa wafanyakazi bora, ikisema hatua hiyo inaleta hamasa na kukuza uchumi wa kampuni hiyo na wa taifa.

Mgeni rasmi wakati wa hafla ya utoaji wa tuzo kwa wafanyakazi bora wa mwaka wa Kampuni ya Simba Supply Chain Solutions Ltd (SSCS) na Simba Logistics Ltd ambazo ni Kampuni tanzu za Simba Bingwa, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alisema:

"Kwa namna ya pekee, niwapongeze wakurugenzi wa Kampuni za Simba Bingwa (Simba Chain, Simba Logistics pamoja na Simba Trailers) kwa kuwa na sera madhubuti za rasilimali watu kwa ustawi wa wafanyakazi wake.

"Ni jambo zuri na la kujivunia. Serikali inajivunia kuwa na waajiri wanaothamini wafanyakazi wao kwani ni rasilimali pekee inayoweza kufanya vitu vitokee na kuleta matokeo mahala pa kazi.

"Mafanikio ya wafanyakazi ni mafanikio ya kampuni kwa sasa na kwa siku zijazo, hivyo niwasihi wafanyakazi kuongeza juhudi na maarifa katika kazi zao na kuwezesha kampuni kufikia malengo makubwa."

Alisema kwa sasa Kampuni za Simba zina wafanyakazi takribani 400 walioajiriwa moja kwa moja. Serikali inatamani kuona ndani ya miaka michache ijayo ajira hizo zinakuwa maradufu kwa kuwa peke yake haiwezi kuwaajiri watanzania wote.

Wakurugenzi wa Kampuni ya Simba Bingwa walisema kuwa katika mwaka 2021, kampuni yao ilianzisha utaratibu wa kupima utendaji kazi kwa wafanyakazi wote wakianza na kundi la madereva ambalo ndilo lilokuwa la kwanza kuingia katika mpango huo.

"Mpango huu tuliouanzisha wa kutoa tuzo kwa madereva bingwa na wafanyakazi umeleta matokeo mazuri sana kwa ustawi wa kampuni na wafanyakazi kwa ujumla.

"Hafla kama hii ilifanyika kwa mara ya kwanza mwezi Machi 2022 ambapo wafanyakazi kutoka idara mbalimbali walizawadiwa ikiwa ni utambuzi wa kampuni kutokana na michango yao iliyotukuka katika kuisongesha Tanzania na Afrika mbele," alisema Ally Dewji, mmoja wa wakurugenzi wa kampuni hiyo.

Mkurugenzi mwenza, Hussein Dewji alisema kampuni yao kwa muda mrefu ilikuwa ikihusika na usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya barabara pamoja na uundaji wa matrela kuwezesha sekta ya usafirishaji lakini hivi karibuni wamepanua wigo wa biashara kwa kuanzisha kitengo cha utoaji mizigo bandarini pamoja uhifidhi wa mizigo katika maghala (Simba Terminals).

Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Omary Kumbilamoto alisema: "Tunazishukuru Kampuni za Simba kwa kuendelea kusaidia maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam, ikiwamo ujenzi wa zahanati, shule na mengine mengi."

Wafanyakazi walioshinda tuzo hizo walisema zimewaongeza ari kujituma zaidi kazini ili kufikia malengo binafsi kitaaluma na kimaendeleo, pia kusaidia kampuni kutimiza malengo yake.

Mwenyekiti wa kampuni hizo, Azim Dewji aliwataka wafanyakazi, hususani madereva, kujenga uzalendo na wanapokuwa nje ya nchi wawe mabalozi wa kutangaza mambo mazuri ya Tanzania.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Joyce Ndalichako, akikabidhi tuzo ya kampuni namba moja inayo zingatia usalama kazini kwa mkuu wa kitengo cha usalama na afya kazini wa Tigo, Dismas Anthony. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# GGML yaja na teknolojia mpya maonyesho ya OSHA

**Na Halfan Chusi**

KATIKA kuadhimisha Siku ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi Duniani - 2023 ambayo kitaifa inafanyika mkoani Morogoro, Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imekuja na teknolojia mpya za kisasa katika kudumisha usalama na afya mahala pa kazi.

Teknolojia hizo mahsusi kwa afya na usalama wa wafanyakazi wanaofanya kazi migodini, zimetajwa kuwa za kipekee kutokana na ubunifu uliotekelezwa na kampuni hiyo na kuleta mageuzi katika uchimbaji madini.

Akifafanua kuhusu ubunifu huo mjini Morogoro katika banda la maonyesho la GGML juzi, Ofisa Mwandamizi wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi, Sospeter Mkombati kuwa mwaka huu wameamua kuja na vitu tofauti.

Alisema GGML kwa miaka mingi iliyoshiriki maonyesha hayo yanayoratibiwa na Wakala wa Afya na Usalama Mahali pa kazi (OSHA), ililenga kuelimisha umma kuhusu masuala ya usalama mahala pa kazi, lakini safari hii inataka kuwafundisha ili wananchi wanaotembelea banda hilo wakalete mageuzi katika kampuni zao.

Alisema teknolojia hizo ambazo GGML imekuja nazo katika maonyesho ya mwaka huu, zinathibitisha kipaumbele cha kwanza cha kampuni hiyo ambacho ni usalama na afya mahali pa kazi.

Mkombati alitaja teknolojia ya kwanza kuwa 'Refugee chamber' ambayo ni chumba maalum cha dharura ambacho huwekwa ndani ya mgodi chini ya ardhi ili kuwawezesha wafanyakazi waliopo ndani ya mgodi kwenda kukusanyika hapo wakati wakisubiri uokozi mwingine kutoka juu.

Aliitaja teknolojia nyingine waliokuja nayo kuwa ni ya mifumo ya kudhibiti ajali za moto kwenye magari ambapo sasa magari yote ya kampuni hiyo ikiwamo mitambo, yamefungwa mifumo hiyo kwenye injini.

Alisema mifumo hiyo ina uwezo wa kutoa maji maalum kuzima moto wowote unaoweza kutokea ndani ya injini ya gari au mtambo bila dereva kuamuru au kushuka kwenye gari kutafuta kifaa cha kuzima moto.

Mkombati aliitaja teknolojia ya tatu ni matumizi ya ndege zisizo na rubani katika kupiga picha na video ndani ya mgodi ili kutambua usalama wa miamba kabla ya mfanyakazi kwenda kuchimba.

Teknolojia nyingine ni ngazi maalum ya uokozi ambayo inatumika kwenye njia ya dharura wakati wa kujiokoa kutoka ndani ya mgodi mbali na njia kuu ya kuingia na kutoka mgodini.

"Ukiacha chumba cha dharura "refugee chamber", GGML imebuni njia ya dharura ambayo ina ngazi za kisasa zinazomwezesha mfanyakazi anayejiokoa kutoka mgodini kupanda ngazi hizo bila kuteleza lakini pia kila baada ya mita sita anaweza kupumzika maana muda mwingine kunaweza kuwa na umbali wa mita 150 kutoka ndani ya mgodi kuja nje," alisema.

Ofisa huyo pia alisema GGML imekuja na choo maalum ambacho kimebuniwa kwa ajili ya kuwasitiri wafanyakazi wanaochimba madini ndani ya mgodi.

Mmoja wa wananchi waliotembelea banda la GGML, Novatus Chuwa alisema amejifunza vitu vingi ambavyo ni vigeni na vinamvutia kuchagua kufanya kazi migodini kwa sababu ya uhakika wa usalama mahali pa kazi.

# PAMBA, KITAYOSCE NGOMA NGUMU KUPANDA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KITENDAWILI cha nani ataifuata JKT Tanzania kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, juzi kilishindwa kuteguliwa, baada ya timu za Pamba na Kitayosce ambazo moja wapo ina nafasi kubwa kushindwa kupata ushindi kwenye mechi zao za Ligi ya Championship.

Timu hizo zimelazimishwa sare kwenye michezo yao zikiwa ugenini, ambapo kila moja ilihitaji ushindi ili kujiweka kwenye mazingira mazuri zaidi.

**Pamba ikiwa kwenye Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya African Sports, huku Kitayosce ikitoka suluhu dhidi ya Fountain Gate kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro.**

Matokeo hayo yanazifanya timu hizo zote mbili kutokuwa na uhakika wa kupanda moja kwa moja kwenye ligi, kwani inahitajika nafasi moja tu kwa sasa baada ya JKT Tanzania kufanikiwa kupanda.

Kwa matokeo hayo timu hizo zimebakisha mechi mbili tu kumaliza msimu wa ligi hiyo, Kitayosce bado iking'ang'ania nafasi ya pili kwa pointi 54, Pamba ikiendelea kuwa nafasi ya tatu kwa pointi 53.

Wakati huo huo, Maafande wa JKT Tanzania wametawazwa kuwa mabingwa wa Ligi ya Championship, baada ya sare ya mabao 3-3 juzi dhidi ya Mashujaa FC, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali, Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam.

Sare hiyo imeifanya kufikisha pointi 63 ambazo sasa haziwezi kufikiwa na timu yoyote, hivyo kuwa rasmi mabingwa wa ligi hiyo ikiwa imebakisha mechi moja na imeshapanda Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itautumikia msimu ujao wa 2023/24.

Mechi nyingine ilichezwa kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea, Mbeya Kwanza ikiibamiza Pan African mabao 2-1.

# Wizara ya Mambo ya Ndani bingwa Mei Mosi

**Na Mwandishi Wetu,** Morogoro

MASHINDANO ya Kombe la Mei Mosi 2023, yamefikia kileleni juzi mjini Morogoro huku timu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ikifanya vizuri katika michezo yake na kuibuka mshindi wa kwanza wa jumla ikifuatiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) na washindi hao kukabidhiwa makombe, medali na vyeti.

Michuano hiyo iliofanyika kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, ilikuwa ni maalum kwa ajili shamrashara za maadhimisho ya Sikukuu ya Wafanyakazi duniani ambayo kilele chake ni leo.

Katika mashindano hayo yalishirikisha timu za mpira wa miguu, netiboli na mchezo wa kuvuta kamba kwa wanaume na wanawake.

Kwa upande wa mpira wa miguu, bingwa ni timu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, mshindi wa pili ni timu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na mshindi wa tatu ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

Kwa upande wa mchezo wa netiboli bingwa ni Ofisi ya Rais Ikulu wakifuatiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, huku nafasi ya tatu ikienda kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, JKT.

Katika mchezo wa kamba kwa wanaume, bingwa ni timu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), mshindi wa pili ni Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na mshindi wa tatu ni Ofisi ya Rais Ikulu wakati kwa upande wa wanawake bingwa ni timu ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), mshindi wa pili ni Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) na mshindi wa tatu ni Wizara ya Afya.

Akifunga mashindano hayo juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Kaspar Mmuya, alisema yamewasaidia watumishi kujenga afya ya mwili na akili, hivyo kwenda kuongeza ari ya kufanya kazi na kutoa huduma stahiki kwa wananchi katika maeneo yao ya kazi.

**GOFU...**



Katibu Mkuu Mstaafu, Ombeni Sefue, akipiga mpira wakati wa mashindano ya Gofu ya Galinoma Memorial Tournament, yaliyofanyika katika viwanja vya Gofu Lugalo, Dar es Salaam juzi, ambapo Kampuni ya The Guardian Limited ni miongoni mwa wadhamini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mogela akunwa na kiwango Simba CAF

**Na Hadija Mngwai**

NYOTA wa zamani wa Simba, Zamoyoni Mogela, amefunguka kuwa, kiwango kilichoonyeshwa na Simba ugenini katika mchezo wa mkondo wa pli robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca ya Morocco, ni cha hali ya juu, ambacho kiliwazidi uwezo wapinzani wao hao licha ya kutolewa.

Simba Ijumaa usiku ilimaliza mwendo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa msimu huu baada ya Wydad kushinda kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-3, kutokana na dakika 90 za michezo miwili kila timu kushinda bao 1-0 nyumbani.

Akizungumza na Nipashe jana, Mogela alisema Simba walifanya vizuri katika mchezo huo jambo lililowasababisha kuwakamata wapinzani licha ya kutolewa kwa dosari ndogo.

"Simba walifanya vizuri kwenye eneo la ulinzi na kiungo, walijitahidi sana, kosa dogo walilolifanya mabeki ndio lilosababisha wapinzani kuweza kufunga, lakini walikuwa wamewakamata sana na kwa ujumla walifanya vizuri ila tatizo lilikuwa mbele kidogo.

"Niwapongeze wachezaji walijitoa na walijituma na katika mchezo lolote linaweza kutokea, wenzao walitumia yale mapungufu yaliyojitokeza, tungekuwa na watu makini tungebadilisha mchezo," alisema Mogela.

# Prisons yaigeukia Kagera Sugar FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kuondoka na pointi tatu ugenini mbele ya Geita Gold FC, Kocha Mkuu wa Tanzania Prisons, Mohammed Abdallah 'Bares', amesema anahitaji alama zingine tatu ugenini katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar.

Tanzania Prisons inapambana kujiondoa katika nafasi ya kucheza Play Off na kushuka daraja, ambapo wiki iliyopita iliibuka na ushindi wa mabao 3-1 kwa kuwafunga Geita Gold nyumbani kwao.

Kwa matokeo hayo Tanzania Prisons imepanda kwa nafasi moja juu na sasa wanashika ya tisa wakiwa na alama 31 sawa na Dodoma Jiji FC ambao wako nafasi ya 10 katika msimamo wa ligi hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Bares alisema malengo yao ni kuhakikisha kila mechi wanapambana kupata alama tatu na kwamba baada ya kushinda dhidi ya Geita Gold FC sasa wanajipanga kwa mechi yao dhidi ya Kagera Sugar.

"Kwa sasa lazima kushinda mechi zetu zote iwe ugenini au nyumbani, muhimu ni kuondoka na pointi kwa sababu waliopo chini yetu wanahitaji kupanda na sisi pia tunahitaji kupanda juu ili kufanikishe hilo lazima ushinde mechi zako," alisema Bares.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WALKER ATAKA KUBAKI

MLINZI wa Manchester City na England, Kyle Walker, 32, anataka kubakia katika klabu hiyo licha ya muda wake mdogo wa kucheza msimu huu na Aston Villa na AC Milan wakimtaka. ***(Star)***

### CITY WAJITOA KWA MOUNT

KLABU ya Newcastle na Manchester City zimejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili Mason Mount, 24, wa Chelsea, huku kiungo huyo wa kati wa England, akitarajiwa kuondoka Stamford Bridge msimu huu wa majira ya joto. ***(Football Insider)***

### ARSENAL YAMTAKA MOUNT

ARSENAL bado ina nia ya kumsajili Mason Mount msimu huu wa majira ya joto jambo ambalo linaweza kumaanisha 'Washikabunduki' hao kusitisha nia yao ya kumsajili kiungo wa kati wa West Ham na England, Declan Rice, 24. ***(Mail)***

### WATKINS ATAKIWA BAYERN

BAYERN Munich inavutiwa na mshambuliaji wa Aston Villa na England, Ollie Watkins, 27, kama mbadala wa mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, 29. ***(Mirror)***

### XHAKA KUPELEKWA SOKONI

ARSENAL itasikiliza ofa kwa kiungo, Granit Xhaka, 30, mlinzi Kieran Tierney (25) na mshambuliaji Folarin Balogun (21), ili kufadhili usajili wa kikosi kikali kwa lengo la kurejea Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mirror)***

### KOKCU AWINDWA VILLA

ASTON Villa ipo mstari wa mbele kumsajili nahodha wa Feyenoord, Orkun Kokcu, 22, msimu huu wa majira ya joto, huku klabu zingine tano za Ligi Kuu pia zikimtaka kiungo huyo wa Uturuki. ***(Mirror)***

### ADARABIOYO ATAJWA INTER

KLABU ya Inter Milan inapanga kumnunua beki wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo, 25, ambaye amebakiwa na zaidi ya mwaka mmoja katika mkataba wake pale Craven Cottage. ***(Sky Sports)***

### SAINT-MAXIMIN AGOMBEWA

KLABU ya Tottenham Hotspur na AC Milan zinawania saini ya winga wa Newcastle United, Allan Saint-Maximin, 26, lakini Magpies wanataka ada ya pauni milioi 50 kwa mchezaji huyo. ***(Mirror)***

### MAGUIRE HOFU JUU UTD

HARRY Maguire,30, anahofia kwamba atalazimika kuondoka Manchester United msimu huu wa majira ya joto huku mlinzi huyo akihofia kupoteza nafasi yake katika kikosi cha England kabla ya Euro 2024. ***(Mail)***

### GUEHI AWANIWA ARSENAL

ARSENAL ina nia ya kumnunua beki wa kati wa Crystal Palace, Marc Guehi, 22. ***(Express)***

### TUDOR AFIKIRIWA JUVE

JUVENTUS inafikiria kumwajiri Kocha wa Marseille, Igor Tudor, iwapo Max Allegri ataondoka msimu huu wa majira ya joto, huku walengwa wengine Antonio Conte na Zinedine Zidane wakionekana kuwa ghali sana ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ANCELOTTI ALINGANISHA UTATU WA KINA BENZEMA NA RONALDO

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alilinganisha upatikanaji wa Karim Benzema na Vinicius Junior na Rodrygo na ule wa Cristiano Ronaldo na Gareth Bale, baada ya hat-trick yake ya kipindi cha kwanza kuisaidia Real Madrid kuwaangusha Almeria, Jumamosi.

**Benzema alihitaji dakika 42 pekee kukamilisha mabao matatu katika ushindi wa 4-2, huku akitengeneza pasi nzuri kwa Vinicius na Rodrygo kabla ya kupiga penalti.**

Rodrygo kisha akaongeza bao la nne, huku mabao ya Lazaro na Lucas Robertone yakihakikisha Almeria inaweka alama ya heshima kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu.

> ●●● Ni watatu tofauti, ila wote ni wazuri, hao wa 2014 walikuwa hatari sana na hao...

Baada ya mchezo huo, Ancelotti aliulizwa ikiwa fowadi watatu wa sasa wa Madrid wanaweza kufikia ya vipaji vya wale walioiwezesha 'Los Blancos' hao kutwaa mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu mitano kati ya 2013-14 na 2017-18.

"Ni swali zuri," alisema Muitaliano huyo.

"Wanafanana kwa ufanisi na ubora, na sifa tofauti za wachezaji.

"Ni watatu tofauti, lakini wote ni wazuri sana. Watatu hao wa 2014 walikuwa hatari sana na watatu hao sasa pia ni hatari sana."

Akiwa pia amefunga pia hat-trick katika ushindi mnono dhidi ya Real Valladolid na Barcelona mwezi huu, Benzema amefunga 'hat-trick' tatu katika mechi nane za Real Madrid.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 567,

MECHI KALI
LEICESTER
VERSUS
EVERTON
1 | 1.98
X | 3.35
2 | 3.50

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI: YAMAL NI MCHEZAJI MAALUM




**BARCELONA,** Hispania

XAVI anaamini Lamine Yamal atakuwa na mafanikio makubwa mbeleni baada ya mchezaji huyo kijana kuweka historia kwa Barcelona katika mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, dhidi ya Real Betis, Jumamosi.

Yamal alitambulishwa kama mbadala wa dakika za lala salama pale Camp Nou wakati Barca ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Betis, na kurejesha uongozi wao wa pointi 11 kileleni.

Nyota huyo ambaye ni zao la akademi ya La Masia, mwenye umri wa miaka 15 na siku 290, aliweka rekodi ya kuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya LaLiga kuichezea Barcelona.

Yamal nusura atengeneze bao la dakika za lala salama na Ousmane Dembele, lakini winga huyo akayumba mbele ya lango, na Xavi anaamini kuwa kiungo huyo ana kipaji cha kufanya vema hapo mbeleni.

Kocha huyo wa Barca alisema: "Nimemwambia ajaribu mambo. Akiwa na umri wa miaka 15, ni kipaji na mchezaji maalum.

"Anaweza kufunga, amesaidia na ukimuona kwenye mazoezi unaona anaweza kuwa mkubwa sana." Raphinha alifunga bao moja na kusaidia jingine katika kipigo cha Betis, huku Andreas Christensen na Robert Lewandowski pia wakifunga na Guido Rodriguez alijifunga.

Winga huyo wa Brazil aliunga mkono maoni ya Xavi kuhusu Yamal, akisema: "Nilipokuwa na umri wa miaka 15, niliichezea timu ya jirani yangu.

"Inashangaza. Ingekuwa ajabu kufunga bao."

Raphinha alipendekeza Barca lazima warudie uchezaji wao kama vile ule dhidi ya Betis, ambao ulikuwa tofauti kabisa na mchezo wao wa Jumatano katika kichapo cha mabao 2-1 kutoka kwa Rayo Vallecano.



# Sterling: Chelsea wana hasira

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Chelsea wapo kwenye wakati mgumu kupata majibu ya mwenendo wao mbaya msimu huu kwa mujibu wa Raheem Sterling.

Lakini akaongeza klabu hiyo ya Ligi Kuu England inaweza kubadilisha maisha yao chini ya kocha sahihi.

Kipigo cha Chelsea cha mabao 2-0 kutoka kwa Brentford Jumatano kiliwaacha nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi, na kuwa katika msimu mbaya zaidi tangu ule wa 1993-94 - walipomaliza nafasi ya 14 chini ya Kocha Glenn Hoddle - licha ya wamiliki wao wapya wa Marekani kutumia fedha nyingi kununua wachezaji.

"Tunasikitika tunapotoka nje ya uwanja na kuhisi hasira na kukata tamaa," alisema Sterling akiambia gazeti la The Sun.

"Kuna wakati tunapomaliza mchezo unakaa tu kwenye chumba cha kubadilishia nguo ukiangalia nafasi kwa sababu unashindwa kuelewa nini kimetokea.

"Ni vigumu kuch
kua. Unajaribu kila ma
kutafuta suluhu chany
Kutakuwa na mazun
umzo, wachezaji wakij
ribu kukubaliana na ki
kilichotokea katika dakil
kumi hivi zilizopita. Si r
hisi."

Chelsea inaongozwa r
kocha wa muda, Fran
Lampard, huku koch
wa zamani wa Totte
ham Hotspur na Par
Saint-Germain, Mauric
Pochettino akionekan
kuwa na nafasi ya kuch
kua nafasi hiyo ya kud
mu.

## HABARI MICHEZO

,947,180

# YANGA U-17 YATOA ONYO LIGI TFF, SIMBA IKIIANZA KWA SARE

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya kwanza ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kwa vijana chini ya miaka 17, iliyoanza Ijumaa iliyopita, imekamilika kwa timu zote 16 kushuka dimbani, huku Yanga ikianza kwa kutoa onyo kwa timu zote zinazoshiriki ligi hiyo, ilipoichakaza African Sports mabao 6-0, mechi ikichezwa Uwanja wa Kituo cha Ufundi TFF, Kigamboni, Dar es Salaam.

Wakati Yanga ikitoa kipigo hicho kikali, Simba ililazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ihefu kwenye mechi nyingine ya ligi hiyo.

**Mabao ya Yanga chini ya miaka 17, yalifungwa na Majid Ismail na Sadiki Mapande, kila mmoja akifunga mawili, Nasri Khalifa na Rashid Abdallah kila mmoja akifunga bao moja.**

Mabao ya Simba chini ya miaka 17, yalifungwa na Hamisi Juma na Hamisi Obeid, huku ya Ihefu yakitiwa kwenye kamba na Athumani Idd na Hamisi Omari.

Mechi nyingine ilikuwa ni kati ya KMC dhidi ya JKT Tanzania ambazo nazo zilitoka sare ya mabao 2-2 kwenye uwanja huo huo.

JKT Tanzania ndiyo iliyoanza kutangulia kufunga mabao mawili kupitia kwa Ivan Hagu na Mohamed Omari, lakini Juma Mashaka na Daniel Barnard waliisawazishia KMC yote mawili baadaye.

Transit Camp nayo ikatoa kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya Green Warriors, wafungaji wakiwa ni Mwarami Salum na Salim Sheck, waliifungia timu hiyo mabao.

Singida Big Stars nayo ilianza ligi hiyo kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya JKU Academy likiwekwa kwenye kamba na Haruna Hamisi, huku Ruvu Shooting ikiishikisha adabu African Lyon kwa mabao 3-1.

Nayo Azam FC ilianza na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, Abdulrazack Ramadhani akijifunga mwenyewe, lingine likiwekwa wavuni na Mohamed Shira, huku Pan African ikikiona cha moto kwa kubugizwa mabao 5-1 dhidi ya Karume Youth Centre, yakiwekwa kwenye kamba na Henry Lyimo, Stanslaus Rafael, Bindo Bakari, Denis Charles na Shame Bakari, la kufutia machozi likifungwa na Paulo Stephen.

**MBIO...**



Wafanyakazi wa Benki ya KCB Tanzania, ambao ni washirika wa Mbio za 'Run 4 Autism Tanzania', zilizofanyika katika viwanja vya Farasi, Oysterbay, Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba sasa kusukwa upya michuano CAF

INATOKA UK. 24

kwangu ndicho muhimu zaidi. Tumepambana vya kutosha, kama tungetumia nafasi mbili kubwa tulizozipata Dar es Salaam, saa hizi tungekuwa nusu fainali, lakini huu ndiyo mpira," alisema Robertinho.

Clatous Chama kwa upande wake alisema walipambana kiasi cha kutosha kwa ajili ya mashabiki, wanachama na familia zao, lakini haikuwa bahati yao.

"Hatuna cha kusema, kweli tumetoka, lakini mimi nashukuru kwa Mungu, viongozi wetu, mashabiki, familia na wote waliokuwa wanatupa sapoti, tumechoka, lakini mimi naona kama tumepambana vizuri tu, haikuwa bahati yetu ni mipango ya Mungu tu, tumshukuru Mungu. Kukosa penalti inaumiza sana, lakini ni mpira hatuwezi kusema mengi na imepita, tutaangalia yale yanayokuja mbele," alisema Chama.

Kwa upande wa Meneja Habari na Mawasiliano ya Klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kufika hatua ya robo fainali mara tatu haina maana Simba imefeli kwa sababu Mamelodi Sundowns, timu inayosifiwa kwa ubora Afrika kwa misimu mitano imekuwa ikiishia robo fainali na sasa wamefanikiwa kutinga nusu.

"Kama Simba tumecheza robo fainali tatu tunaambiwa tumefeli vipi hao walicheza mara tano na msimu huu kufanikiwa, bado tuna sababu ya kujivunia kwa hapa tulipofikia na kusahihisha makosa yetu na kujifunza kutokana na wenzetu.

"Ili kutoka hapa lazima tufanye juhudi kila linalowezekana na kufanya usajili wa wachezaji bora na wenye uwezo wa kuipeleka Simba nusu fainali," alisema Ahmed.

Aidha, Ahmed alisema kikosi kinatarajia kuondoka jijini Dar es Salaam leo kuelekea Ruangwa mkoani Lindi kwa ajili ya mechi ya ligi dhidi ya Namungo FC, itakayopigwa keshokutwa katika Uwanja wa Majaliwa, na nusu fainali ya Kombe la FA, Jumamosi wiki hii kwenye Dimba la Nangwanda Sijaona, mkoani Mtwara.



# JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/05/23 | 20:00 | Mjallby vs AIK Football | 2.77 | 2.93 | 2.45 |
| 02. 03/05/23 | 20:00 | Sparta Prague vs Slavia Prague | 2.31 | 3.22 | 2.80 |
| 03. 03/05/23 | 20:00 | Panathinaikos vs PAOK | 2.29 | 2.98 | 3.30 |
| 04. 03/05/23 | 20:30 | Valencia vs Villarreal | 2.90 | 3.30 | 2.26 |
| 05. 03/05/23 | 21:45 | Stuttgart vs Eintracht Frankfurt | 2.42 | 3.39 | 2.85 |
| 06. 03/05/23 | 21:45 | Burton vs Cambridge Utd | 2.97 | 3.22 | 2.31 |
| 07. 03/05/23 | 23:00 | Getafe vs Celta Vigo | 2.50 | 2.90 | 2.90 |
| 08. 04/05/23 | 01:00 | CD Palestino vs San Lorenzo | 2.90 | 3.01 | 2.36 |
| 09. 04/05/23 | 03:00 | Colo Colo vs Boca Juniors | 2.37 | 3.08 | 2.83 |
| 10. 04/05/23 | 03:00 | Club Guarani vs SC Emelec | 2.37 | 3.11 | 2.80 |
| 11. 04/05/23 | 20:00 | Norrkoping vs Hammarby | 2.52 | 3.33 | 2.42 |
| 12. 04/05/23 | 21:45 | Empoli vs Bologna | 2.95 | 3.10 | 2.33 |
| 13. 04/05/23 | 21:45 | Huddersfield vs Sheffield Utd | 2.45 | 3.20 | 2.70 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATATU - 01/05/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 4108 | Como vs Palermo | 2.09 | 3.24 | 3.29 |
| 15:00 | 1687 | Universitatea Cluj vs Voluntari | 1.99 | 3.18 | 3.65 |
| 15:00 | 2355 | Alashkert Martuni vs Lernayin Artsakh | 1.29 | 4.66 | 8.90 |
| 15:00 | 2357 | Rotherham vs Middlesbrough | 3.36 | 3.31 | 2.04 |
| 15:00 | 3093 | Welayta Dicha FC vs Legetafo Legedadi | 1.50 | 3.85 | 5.82 |
| 15:00 | 3968 | Sioni Bolnisi vs Loko Tbilisi | 1.38 | 4.46 | 6.64 |
| 15:50 | 3788 | Al Seeb vs AL Etihad | 1.25 | 4.50 | 8.80 |
| 16:00 | 1129 | Sudtirol vs Genoa | 3.82 | 3.08 | 1.99 |
| 16:00 | 1182 | Falkenbergs vs Ljungskille | 1.46 | 4.21 | 5.34 |
| 16:00 | 1513 | Utsiktens BK vs Orgryte IS | 2.32 | 3.42 | 2.89 |
| 16:00 | 2527 | Brescia vs Cosenza | 1.88 | 3.28 | 3.96 |
| 16:00 | 2728 | Bari vs Cittadella | 2.01 | 3.09 | 3.72 |
| 16:00 | 2807 | IFK Goteborg vs Norrkoping | 2.49 | 3.19 | 2.54 |
| 16:00 | 3569 | Kaizer Chiefs vs Moroka Swallows FC | 1.80 | 3.20 | 4.52 |
| 16:00 | 3704 | Trelleborgs FF vs GIF Sundsvall | 1.92 | 3.51 | 3.77 |
| 16:00 | 4048 | Benevento vs Parma | 3.24 | 3.13 | 2.16 |
| 16:00 | 5067 | Solin vs Orijent Rijeka | 1.96 | 3.19 | 3.50 |
| 16:00 | 5325 | Ascoli vs Pisa | 2.46 | 3.03 | 2.83 |
| 17:00 | 1141 | St Patricks vs Sligo Rovers | 1.99 | 3.24 | 3.34 |
| 17:00 | 4144 | Lokomotiva Zagreb vs HNK Gorica | 1.92 | 3.34 | 3.44 |
| 17:15 | 5432 | Sporting Gijon vs Lugo | 1.50 | 3.69 | 6.59 |
| 18:00 | 2849 | Fasil Kenema vs Hadiya Hosahina FC | 2.18 | 2.79 | 3.52 |
| 18:00 | 3749 | Artsakh vs Bkma Yerevan | 1.90 | 3.27 | 3.74 |
| 19:00 | 1314 | UCD Dublin vs Dundalk FC | 4.53 | 3.45 | 1.67 |
| 19:00 | 1655 | Valerenga vs Lillestrom | 2.52 | 3.32 | 2.59 |
| 19:00 | 1936 | Venezia vs Modena | 2.19 | 3.19 | 3.14 |
| 19:00 | 2241 | Ujpest FC vs Ferencvaros TC | 4.88 | 3.89 | 1.57 |
| 19:00 | 2894 | Bohemians FC vs Cork City | 1.74 | 3.45 | 4.07 |
| 19:00 | 4325 | Drogheda Utd vs Shelbourne | 2.73 | 2.99 | 2.44 |
| 19:00 | 4465 | Zira vs Turan Tovuz | 1.79 | 3.27 | 4.26 |
| 19:05 | 3793 | Najran SC vs AL Qaisoma | 2.57 | 2.88 | 2.67 |
| 19:10 | 2362 | Slaven Belupo vs HNK Rijeka | 3.08 | 3.13 | 2.15 |
| 19:20 | 4492 | AL Hazm vs Al Faisaly (KSA) | 1.94 | 3.00 | 3.45 |
| 19:30 | 1180 | Malaga vs Huesca | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 19:30 | 1810 | Blackburn vs Luton Town | 2.23 | 3.30 | 2.95 |
| 19:45 | 1814 | Arsenal W vs Wolfsburg W | 2.44 | 3.37 | 2.54 |
| 20:00 | 1466 | Istanbulspor vs Giresunspor | 2.37 | 3.36 | 2.73 |
| 20:00 | 3520 | Real Sporte vs Vitoria Setubal | 2.33 | 3.21 | 2.79 |
| 20:00 | 4848 | Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.45 | 2.90 | 2.20 |
| 20:00 | 5282 | Midtjylland vs Silkeborg | 1.72 | 3.64 | 4.56 |
| 20:30 | 1829 | Rapid Bucuresti vs CFR Cluj | 3.02 | 3.13 | 2.27 |
| 20:30 | 2079 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Haifa | 2.57 | 3.29 | 2.40 |
| 21:15 | 1058 | Derry City vs Shamrock Rovers | 2.31 | 3.08 | 2.83 |
| 21:30 | 2143 | Frosinone vs Reggina | 1.67 | 3.47 | 4.94 |
| 21:45 | 2226 | Sochaux vs Dijon | 1.80 | 3.25 | 4.40 |
| 22:00 | 2086 | Leicester vs Everton | 1.98 | 3.35 | 3.50 |
| 22:00 | 2452 | Sevilla FC vs Girona | 1.95 | 3.40 | 3.55 |
| 22:00 | 4307 | Londrina PR vs Criciuma SC | 2.68 | 2.83 | 2.68 |
| 22:00 | 4669 | Burgos vs Villarreal B | 2.19 | 3.00 | 3.35 |
| 23:00 | 1315 | Envigado FC vs Atletico Huila | 2.01 | 3.15 | 3.52 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Mei 1, 2023

Nipashe




Sterling: Chelsea wana hasira UKURASA 22

# Yanga yaweka rekodi

## ●●● Yatinga nusu fainali Shirikisho Afrika, sasa kukutana na Marumo ya Sauzi, taa za Uwanja wa Mkapa ni shida...

**Na Adam Fungamwango**

HISTORIA imeandikwa jana Klabu ya Yanga baada ya kufanikiwa kutinga nusu fainali ya Kombe la Shirikisho barani Afrika tangu kuanzishwa kwake miaka 88 iliyopita.

**Ikiwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, pamoja na kulazimishwa suluhu, imetinga hatua hiyo kwa ushindi wa mabao 2-0 ilioupata ugenini Jumapili ya Aprili 23, mwaka huu kwenye Uwanja wa Godswill Akpabio nchini Nigeria.**

Inakuwa ni klabu ya pili nchini kutinga hatua ya michuano ya kombe hilo, baada ya Simba kufanya hivyo mwaka 1993 ilipoifunga Al Harrach ya Algeria kwa jumla ya mabao 3-2, ikishinda 3-0 nyumbani na kufungwa 2-0 ugenini, ikafanikiwa kutinga hatua hiyo, wakati huo likiitwa Kombe la CAF na ikiishia fainali ilipofungwa na Stella Abidjan ya Ivory Coast kwa mabao 2-0.

Mchezo wa kwanza Simba ilipata sare ugenini na kufungwa nyumbani mabao 2-0 Uwanja wa Taifa (sasa Uhuru), Dar es Salaam mbele ya aliyekuwa Rais wa Tanzania wakati huo, Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa mgeni rasmi.



Kiungo wa Yanga, Mudathiri Yahya, akimtoka kiungo wa Rievers United, Chukwu Ugochukwu Morice, kwenye mechi ya mkondo wa pili robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa sare tasa. **MPIGAPICHA WETU**

Kwa matokeo hayo ya jana Yanga sasa itacheza nusu fainali dhidi ya Marumo Gallants ya Afrika Kusini ambayo jana iliifunga Pyramids ya Misri bao 1-0 kwenye Uwanja wa Royal Bafokeng nchini humo.

Gallants inafuzu hatua ya nusu kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya timu hiyo, mchezo uliochezwa Aprili 23, mwaka huu nchini Misri.



Mechi ya nusu fainali kati ya Yanga dhidi ya Marumo Gallants inayoshika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Sauzi ikiwa na pointi 28 kwa mechi 27 ilizocheza, itachezwa Mei 10, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na marudiano yatakuwa nchini Afrika Kusini Mei 17, mwaka huu.

Yanga ilianza mechi hiyo ikionekana kulinda ushindi ilioupata nchini Nigeria na kucheza kwa uangalifu na taratibu, huku Rivers United ikionekana kuwa na haraka ya kusaka bao la mapema.

Hata hivyo, walikuwa ni Yanga walipokaribia kufunga bao dakika ya 12, likiwa ni shambulio kali la kwanza kwenye mchezo huo.

Alikuwa ni Fiston Mayele aliyemtilia pasi ya upendo Clement Mzize, lakini mguso wake wa kwanza kwenye mpira ulikuwa mrefu zaidi, huku kipa Voctor Sichoma, akiwa ametoka kulipunguza lango, akapiga pembeni, wakati mashabiki wa Yanga wakiwa wamesimama wakisubiri kushangilia.

Mzize tena, alikosa bao lingine dakika 10 baadaye, alipoukuta mpira uliokuwa ukizagaa kutokana na purukushani. Aliachia shuti kali lililopaa juu ya lango akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga bao.

Saa moja na dakika 27 kwa saa za Afrika Mashariki na Kati, ikiwa ni dakika ya 27 ya mchezo, baadhi ya taa za uwanja huo zilizimika, zingine kupungua nguvu kama ilivyotokea Machi 28, mwaka huu kwenye mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kati ya wenyeji Tanzania, Taifa Stars dhidi ya Uganda, The Cranes.

Mechi ya Taifa Stars na Uganda ilisimama katika dakika ya 37, na iliendelea tena baada ya mambo kukaa vema dakika 35 baadaye, lakini kwenye mechi ya jana mwanga wa taa ulirejea tena na mchezo ukaendelea saa 20:00 usiku, ikiwa ni baada ya dakika 33 kupita.

Dakika mbili tu baada ya mechi kurejea kuchezwa tena, Rivers United ilifanya shambulizi kali, lakini krosi ya Onoja Joseph ilikosa muunganishaji.

Hali kama hiyo ilitokea tena dakika ya 42, Onoja tena 'alipomwaga maji', lakini wenzake, Nyima Nwagua na Chukwu Morice, waliukosa mpira, ukaambaa pembeni mwa uwanja.

Kipindi cha pili kila timu ilifanya mabadiliko, lakini hakuna kilichoendelea zaidi ya kosakosa za mabao, Mayele mfungaji wa mabao mawili katika mechi ya ugenini, akikosa mara tatu katika nafasi ya wazi, dakika ya 50, 51 na 56.

## Simba sasa kusukwa upya michuano CAF

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa Simba kikirejea nchini jana kutoka Morocco na kupokewa kwa shangwe kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Ndege wa Julius Nyerere, Afisa Mtendaji Mkuu wake, Imani Kajula, ameahidi kusuka timu tishio ambayo anaamini itakwenda kufuzu hatua ya nusu fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

Licha ya kutolewa kwenye hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mabingwa Watetezi, Wydad Athletic Club ya Casablaca, Morocco kwa mikwaju ya penalti 4-3, wanachama na mashabiki wa timu hiyo walijitokeza kwa wingi, wakiwa na ngoma na zana zingine za muziki kwa ajili ya mapokezi yaliyowashangaza viongozi, wachezaji na makocha.

"Niseme tu, mpira wa Tanzania unapiga hatua kubwa Afrika, leo hii tumeondoka Morocco, kila mtu anaisifu Simba na kila mtu anasifu mpira wa Tanzania, lakini hili lisitufanye tukabweteka, ila tulione kama ni changamoto ya kufanya vema zaidi. Na sisi kama klabu hilo ndilo lengo letu, hii ni sehemu ya kujipimia na ninavyokwambia tunakwenda kusuka kikosi zaidi ili tuje kushindana vizuri zaidi kipindi kijacho.

"Uzuri ni kwamba michuano ya Super Cup inaanza wakati wa msimu mpya wa ligi na michuano mingine, kwa hiyo tuna ripoti ya mwalimu, wataalam wachambuzi na waangalizi wa soka kwa ajili ya kuboresho kikosi, na tumeona kuna maeneo ya kuyafanyia kazi na tutayafanyia kazi kweli bila matatizo yoyote," aliahidi Afisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo mara baada ya kuwasili uwanjani hapo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Roberto Oliveira aliwapongeza wachezaji wake kwa kiwango kikubwa walichokionyesha kiasi kwamba mabingwa watetezi walilazimika tu kuomba Mungu ili wafuzu.

"Nawapongeza wachezaji wangu, wamecheza kwa kiwango kikubwa, siwezi kusema kuhusu penalti, lakini kila mmoja ameshuhudia kilichotokea, kiwango cha uchezaji

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042